# KUCHUNGUZA DHAMIRA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA KATIKA *SIKU YA WATENZI WOTE*

**ALI OMAR ALI**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI (M.A KISWAHILI- FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo "***Kuchunguza Dhamira katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Siku ya Watenzi Wote*"** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

**…………………………………………….**

**Dkt. Mohamed Oamry Maguo**

**(Msimamizi)**

**Tarehe:..........................................**

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

# TAMKO

Mimi, **ALI OMAR ALI**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

Saini:……………………………..

Tarehe………………………………

## TABARUKU

Kazi hii, ninatabaruku kwa wazazi na walezi wangu, familia yangu na walimu wangu wote walionisomesha kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu.

## SHUKURANI

Awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kunijaalia afya njema katika kipindi chote cha maisha yangu na katika masomo yangu. Kwa hakika ni kutokana na baraka za zake ndio maana leo hii nimefika katika hatua hii. Pia, ninamshukuru sana kwa kuijaalia familia yangu kuwa na amani, upendo na amani katika kipindi chote nilipokuwa masomoni.

Pia, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa mwalimu na msimamizi wangu Dkt. Mohamed Omary Maguo kwa kuniongoza vema katika hatua zote za utafiti wangu na masomo kwa jumla. Kwa hakika mwalimu wangu umenifunza mengi ambayo nitayazingatia katika maisha ili kuweza kuishi na watu wote kwa hekima na busara. Pia, nitajitahidi kuwa na moyo wa kujitolea katika kusaidia watu wengine ili nao waweze kufika katika hatua kama yangu na ikiwezekana wafike mbele zaidi ya hatua hii.

Napenda pia kuishukuru familia yangu yote ikiwa ni pamoja na wake zangu na watoto wangu wapendwa kwa moyo wao wa uvulivu na kunitia moyo katika kipindi chote cha masomo yangu. Ilikuwa wakati fulani sina muda wa kukaa nao na kuzungumza kwa tua kutokana na kuwa katika harakati za masomo, lakini walivumilia na hawakuwahi kulalamika hata mara moja. Nasema asante sana kwa familia yangu na Allah awabariki sana.

# IKISIRI

Mada ya utafiti ni kuchunguza dhamira katika riwaya ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* ya mtunzi Shaaban Robert. Malengo mahususi ya utafiti yalikuwa mawili ambayo ni kuchambua dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* na kuelezea uhalisia wa dhamira za siku ya Watenzi Wote kwa jamii ya leo. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka na kuchambuliwa kwa kutumika mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa riwaya teule ina dhamira nyingi na sisi tumebainisha dhamira 7 ikiwa ni wasiwasi, ukoloni, malezi, kutimiza wajibu, umuhimu wa elimu na uzalishaji mali. Dhamira hizi zote zinaonekana kuwa zina lengo moja kuu la kumfanya binadamu kujitambua na kuweza kutekeleza majukumu yake ili kujiletea maendeleo katika jamii. Kisaikolojia dhamira hizi ni hai na kwamba licha ya riwaya husika kuandikwa takribani miaka 50 iliyopita lakini bado dhamira zake ni muafaka kwa kizazi cha leo na hata vizazi vijavyo. Uandishi wa aina hii ni wa hali ya juu sana ambao tunauona kwa mwandishi huyu pekee ukimlinganisha na waandishi wengine wa riwaya na fasihi ya Kiswahili kwa jumla. Mwishoni mwa tasinifu hii kumtolewa mapendekezo kwa ajili ya utafiti wa baadaye.

## YALIYOMO

UTHIBITISHO .......... i

HAKIMILIKI .......... ii

TAMKO .......... iii

TABARUKU .......... iv

SHUKURANI .......... v

IKISIRI .......... vi

YALIYOMO .......... vii

**SURA YA KWANZA .......... 1**

**UTANGULIZI .......... 1**

1.0 Utangulizi .......... 1

1.1 Tatizo la Utafiti .......... 4

1.2 Malengo ya Utafiti .......... 4

1.2.1 Lengo Kuu .......... 4

1.2.2 Malengo Mahususi .......... 4

1.3 Maswali ya Utafiti .......... 5

1.4 Umuhimu wa Utafiti .......... 5

1.5 Mipaka ya Utafiti .......... 6

1.6 Mpangilio wa Tasinifu .......... 6

**SURA YA PILI .......... 7**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA .......... 7**

2.0 Utangulizi .......... 7

2.1 Historia Fupi ya Riwaya ya Kiswahili .......... 7

2.2 Dhamira katika Riwaya ya Kiswahili ........................................................ 9
2.3 Kazi Tangulizi juu ya Riwaya za Shaaban Robert ........................................ 13
2.4 Mkabala wa Kinadharia ........................................................................ 15
2.4.1 Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ........................................................ 15
2.5 Hitimisho ................................................................................................ 18

**SURA YA TATU ........................................................................................ 19**

**MBINU ZA UTAFITI ................................................................................... 19**

3.0 Utangulizi ................................................................................................ 19
3.1 Usanifu wa Utafiti .................................................................................... 19
3.2 Kundi Lengwa .......................................................................................... 20
3.3 Sampuli na Usampulishaji ........................................................................ 20
3.4 Aina ya Data Zilizokusanywa .................................................................. 21
3.4.1 Data za Msingi ....................................................................................... 21
3.4.2 Data za Upili .......................................................................................... 21
3.5 Mbinu za Kukusanyia Data ...................................................................... 22
3.5.1 Usomaji Makini ...................................................................................... 22
3.5.2 Upitiaji wa Nyaraka ............................................................................... 22
3.6 Uchambuzi wa Data .................................................................................. 23
3.6.1 Mkabala wa Kimaelezo ......................................................................... 23
3.7 Kuaminika na Usahihi wa Data ................................................................ 23
3.8 Maadili ya Utafiti ..................................................................................... 24
3.9 Hitimisho ................................................................................................ 24

**SURA YA NNE ......................................................................................... 25**

**UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI... 25**

4.0 Utangulizi ........................................................................................ 25

4.1 Historia ya Shaaban Robert na Muhtasari wa *Siku ya Watenzi Wote* ............ 25

4.2 Dhamira katika *Siku ya Watenzi Wote* na Uhalisia Wake.............................. 27

4.2.1 Wasiwasi ........................................................................................ 27

4.2.2 Ukoloni........................................................................................... 31

4.2.3 Malezi............................................................................................. 35

4.2.4 Umasikini ........................................................................................ 37

4.2.5 Wajibu............................................................................................ 42

4.2.6 Umuhimu wa Elimu ........................................................................... 44

4.2.7 Uzalishaji Mali .................................................................................. 47

4.3 Hitimisho.......................................................................................... 48

**SURA YA TANO............................................................................................ 50**

**HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO.......................................... 50**

5.0 Utangulizi ........................................................................................ 50

5.1 Muhtasari.......................................................................................... 50

5.1.1 Dhamira katika Riwaya Teule na Uhalisia wake .......................................... 50

5.2 Hitimisho.......................................................................................... 53

5.3 Mapendekezo ..................................................................................... 54

**MAREJELEO ................................................................................................ 55**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Riwaya ya Kiswahili sio utanzu mkongwe ukilinganisha na ushairi wa Kiswahili ambao una historia ndefu sana katika Pwani ya Afrika ya Mashariki. Hii haina maana kuwa riwaya ni utanzu mpya kabisa ambao haujapata kuwepo katika jamii la hasha bali ni utanzu mpya kwa maana ya maandishi na kuwekwa katika kitabu kama ilivyo hivi sasa. Riwaya ya Kiswahili ilitokana na hadithi bunilizi, tarihi, visasili, ngano, soga na vigano ambavyo vimekuwepo katika jamii vikisimuliwa tangu karne na karne (Madumulla, 2009). Vijitanzu hivi vya fasihi simulizi hayakuwahi kuwekwa katika mandishi bali ni masimulizi ambayo yalikuwa yakirithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine.

Senkoro (1977) anaeleza kuwa riwaya ya Kiswahili ilianza kuandikwa kuanzia karne ya 19 hususani mara baada ya ujio wa wakoloni ambapo uliingiza teknolojia ya uchapishaji katika makoloni. Hii ilitokana na mahitaji ya wakati huo ambapo kulihitajika kuwa na utanzu ambao unasawiri mambo kwa kina zaidi na mambo mtambuka katika jamii. Kwa upande wa riwaya ya Kiswahili inatajwa kuwa riwaya za kwanza za Kiswahili kuandikwa ni zile za Shaaban Robert za *Maisha Yangu* na baadae ile ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (Mlacha na Madumulla, 1991). Riwaya hii ya Shaaban Robert ilisawiri kwa undani maisha ya wakati wa ukoloni kutokana na mtunzi kuwa sehemu ya wanajamii waliopata fursa ya kuishi katika kipindi cha ukoloni na pia alikuwa ni mtumishi katika serikali ya kikoloni. Njogu na Chimerah (1999) kwa upande wao wanadai kuwa riwaya ya kwanza ya

Kiswahili kuandikwa ni ile ya *Uhuru wa Watumwa* iliyoandikwa na Mbotellah mnamo mwaka 1934.

Kimsingi maelezo haya tunakubaliana nayo kuwa riwaya za Shaaban Robert na pia ile ya *Uhuru wa Watumwa* ya Mbotellah zote ziliandikwa katika kipindi cha ukoloni na zinaweza kutazamwa kama riwaya za kwanza za Kiswahili kuandikwa na Waswahili wenyewe. Kimsingi, kazi za waandishi hawa wawili zilifungua pazia la uandishi wa kazi nyingine nyingi za Riwaya ya Kiswahili ambapo Shaaban Robert binafsi aliandika riwaya kuntu. Miongoni mwa riwaya zake ni pamoja na *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Adili na Nduguze*, *Utu Bora Mkulima*, *Siku ya Watenzi Wote* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* kuzitaja kwa uchache. Kutokana na ufundi na ujuzi mkubwa uliotumiwa na mtunzi katika riwaya zake wataalamu mbalimbali wamevutiwa na hatimaye kufanya utafiti wao katika riwaya hizo kama ifuatavyo:

Chuachua (2011) alifanya utafiti wa kuchunguza itikadi katika riwaya za Shaaban Robert na kubaini kuwa ndani ya riwaya za nguli huyu kuna itikadi mbalimbali zenye lengo la kujenga jamii nzuri katika taifa. Miongoni mwa itikadi alizozibaini ni pamoja na kuheshimu utu wa binadamu, binadamu wote ni sawa, dini ni njia ya kumjenga mtu katika mambo mema, itikadi ya kuleta mapinduzi kama njia ya kufanikiwa, upendo na mapenzi miongoni mwa wanajamii. Itikadi hizi zililenga katika kuwafanya wanajamii kujitambua na hususani wale waliokuwa wakinyonya katika utawala wa kikoloni walipaswa kuchukua hatua ili kujinasua kutoka katika dhuluma ya unyonyaji waliokuwa wakifanyiwa na wakoloni.

Maelezo ya Chuachua yanaungwa mkono na Ambrose (2014) ambaye alichunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Katika utafiti huu

alibainisha kuwa, mtunzi ameisawiri jamii chini ya uongozi kikoloni ambapo viongozi walikuwa ni watawala waliofanya mambo ya kuwakandamiza wananchi ikiwa ni pamoja na kunyonya nguvu kazi yao na rasilimali zao. Riwaya hizi mbili zilitumia mandhari ya kidhahania lakini lengo kubwa lilikuwa ni kuhakikisha kwamba wanajamii wanapata ujumbe bila ya mkoloni kujua kama ni yeye anasemwa na hata akijua basi inakuwa si rahisi kumchukulia hatua za kisheria mtunzi. Hii ni kwa sababu hakuna mahali ambapo serikali ya kikoloni ilitajwa moja kwa moja. Mtindo huu wa uandishi wa riwaya umemfanya Shaaban Robert kuwa miongoni mwa watunzi wachache wa fasihi ya Kiswahili ambao wanasifika ndani na nje ya Bara la Afrika.

Kimsingi, sisi pia ni miongoni mwa watafiti ambao tumevutiwa sana na utunzi wa riwaya wa Shaaban Robert na kuona kuwa ipo haja ya kuchunguza dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1968 ikiwa ni baada ya Shaaban Robert kufariki dunia. Pamoja na yote yaliyotuvutia kuchunguza riwaya hii ni pamoja na makala ya Mohamed (2006) ambaye alichunguza mtindo katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* na kubainisha mitindo mbalimbali. Mtindo uliotuvutia ni ule wa matumizi ya uwili ambapo Shaaban Robert alikuwa akitaja kila kitu kwa uwili wake ambapo kila alipotaja msikiti alitaja kanisa, alipomtaja shehe alimtaja padre na alipotaja umasikini alitaja utajiri na kuendelea na mtindo huu kwa namna mbalimbali. Baada ya kusoma makala hiyo, tulipata fikira ya kuchunguza dhamira katika riwaya hii inayotajwa kuwa na mtindo wa kipekee katika uteuzi wake wa maneno. Hivyo, tumefanya utafiti wa kuchunguza dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi* wote ya Shaaban Robert.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Shaaban Robert alipata kuishi na kufanya kazi katika kipindi cha utawala wa kikoloni na alifariki dunia mwaka 1962 muda mfupi tu baada ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika. Mtunzi huyu ameacha riwaya na kazi mbalimbali za fasihi ambazo kwazo zimesheheni utajiri mkubwa wa mafunzo yenye adili kwa jamii. *Siku ya Watenzi Wote* ni riwaya inayotajwa kuwa na mtindo wa kipekee wa matumizi ya uwili kwa kila kinachotajwa. Jambo hili limetuvutia sana na hatimaye kutaka kufahamu ni dhamira zipi hasa zinazosawiriwa katika riwaya hii yenye mtindo wa kipekee na ni upi uhalisia wa dhamira hizo kwa jamii ya leo?

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahususi mawili na yamewasilishwa katika sehemu inayofuata:

### 1.2.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*.

### 1.2.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:

i. Kuchambua dhamira katika riwaya teule ya *Siku ya Watenzi Wote* ya Shaaban Robert.

ii. Kuelezea uhalisia wa dhamira za riwaya teule ya *Siku ya Watenzi Wote* ya Shaaban Robert kwa jamii ya leo.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na maswali mawili ambayo ni haya hapa chini:

i. Ni dhamira zipi zinazojitokeza katika riwaya teule ya *Siku ya Watenzi Wote* ya Shaaban Robert?
ii. Dhamira zinazojitokeza katika riwaya teule ya *Siku ya Watenzi Wote* ya Shaaban Robert ina uhalisia gani kwa jamii ya leo?

## 1.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na eneo la kiuchambuzi ambapo kwa kuchambua dhamira za riwaya hii tutatoa faida kubwa kwa wanataaluma na wanajamii kwa jumla kujifunza mambo mazuri ya kutoka katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*. Si mara nyingi kusikia watu wakitaja riwaya hii kuwa ni moja kati ya riwaya zenye mambo mazuri ya kutafitiwa. Hivyo, kupitia utafiti huu tutaweka msingi imara kwa wanataaluma kuifahamu kazi hii kwa mawanda na kuvutiwa kufanya utafiti zaidi wa kuichunguza riwaya hii.

Kwa upande wa nadharia, utafiti huu utajenga msingi imara wa kinadharia katika kufahamu dhamira na uhalisia wake katika jamii hususani kwa kutumia mkabala wa nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Shaaban Robert ni mtaalamu wa kucheza na saikolojia ya wasomaji wake na kwa kutumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi tutaweza kuibua faida kubwa ya utajiri wa dhamira zilizopo katika riwaya hii.

Kijamii, utafiti huu umechambua masuala mbalimbali yenye kuonyesha namna jamii inavyopaswa kuishi, hususani suala la wasiwasi ambalo linatajwa kuwa ni muhimu katika kuleta maendeleo kwa jamii. Riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* imeanza

kueleza suala la la binadamu na wasiwasi mwanzoni tu mwa riwaya hiyo. Hii inaonyesha kwamba maendeleo katika jamii hupatikana pale tu jamii inapotumia wasiwasi kama fursa badala ya kurudi nyuma na kutumia wasiwasi kama ugonjwa. Waswahili wana msemo wao unaosema, “wasiwasi ndiyo akili.”

## 1.5 Mipaka ya Utafiti

Shaaban Robert ni mwandishi maarufu wa kazi za fasihi ya Kiswahili ikiwemo riwaya na ameandika riwaya kama vile *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Utu Bora Mkulima*, *Adili na Nduguze*, *Wasifu wa Siti Binti Saad* na *Siku ya Watenzi Wote* kutaja kwa uchache. Kwa minajili ya kutimiza malengo ya utafiti huu tumeteua riwaya moja tu ya *Siku ya Watenzi Wote* ambayo tunaichunguza katika kipengele cha dhamira tu. Baada ya kuzichambua dhamira husika tumeelezea uhalisia wake kwa jamii ya leo.

## 1.6 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii imeundwa kwa sura tano ambapo sura ya kwanza inahusu utangulizi. Katika sura hii kumewasilishwa vipengele mbalimbali kama vile usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasinifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia na sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti zikihusisha usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa; data za msingi na upili, mbinu za kukusanyia data; usomaji makini na upitiaji wa nyaraka, mbnu za uchambuzi wa data; mkabala wa kimaelezo, usahihi wa data na maadili ya utafiti. Sura ya nne ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti na sura ya tano ni hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inapitia kazi tangulizi ambazo zimefanywa kuhusiana na mada ya utafiti kwa lengo la kubainisha pengo la maarifa. Tumeanza kwa kueleza kwa muhtasari juu ya historia fupi ya riwaya ya Kiswahili na kisha kufanya mapitio kuhusu dhamira katika riwaya na mwisho tumewasilisha kuhusu mkabala wa kinadharia ambapo tumeongozwa na nadharia ya Saikolojia Changanuzi.

## 2.1 Historia Fupi ya Riwaya ya Kiswahili

Riwaya ya Kiswahili ni utanzu wa fasihi andishi ambao umepiga hatua kubwa ya maendeleo kuanzia karne ya 19 mpaka sasa. Ni katika kipindi hicho ndipo riwaya ilianza kuandikwa na kuwasilishwa katika machapisho kama tunavyoona leo hii. Mlacha na Madumulla (1991) wanaeleza kuwa, riwaya ya Kiswahili ilianza kuonekana mara baada ya Shaaban Robert kuandika *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* ikiwa ni riwaya iliyoelezea maisha yake na namna alivyoishi na kufanya kazi katika serikali ya kikoloni. Njogu na Chimerah (1999) wao wanaeleza kuwa riwaya ya Kiswahili ilianz pale Mbotela alipoandika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* mnamo mwaka 1934. Kimsingi, kwa vyovyote vile iwavyo, hawa ndio waandishi wa kwanza wa riwaya za Kiswahili kwani kabla ya hapo hakukuwa na riwaya iliyofuata mtindo kama huu.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa historia ya riwaya imeanzia katika fani za kijadi kama ngano, visasili, tarihi, vigano na tendi ambazo zilikuwa katika masimulizi na

hazikuwa zimeandikwa. Kilichofanyika mara baada ya kugunduliwa kwa maandishi ni kuchukua masimulizi ambayo tayari yalikuwepo na kuyaweka kwenye mfumo wa maandishi. Maelezo haya ni sahihi na tunakubaliana nayo kwa kiasi kikubwa kwa sababu yanaeleza uhalisia wa mambo. Wageni walipokuja katika nchi za Afrika na kuanza kufundisha kusoma na kuandika walileta hoja kuwa Afrika haikuwa na riwaya mpaka walipokuja wao na kuianzisha. Katika hali ya kawaida ni kweli kuwa wao walileta maandishi lakini kudai kwamba ndio waanzilishi wa riwaya ya Kiswahili sio jambo la kweli (Madumulla, 2009).

Mawazo kwamba, chimbuko la riwaya ya Kiswahili ni fani za kijadi za kiafrika za fasihi simulizi yanaungwa mkono na Madumulla (2009) ambaye anasema kuwa fasihi simulizi ndio chimbuko la fasihi andishi ikiwemo riwaya. Anasema kuwa riwaya ilitokana na ngano ambazo bibi na babu walikuwa wakiwasimulia wajukuu zao usiku wakiwa wanaota moto. Hadithi za Paukwa Pakawa ambazo watoto wamekuwa wakisimuliwa na bibi au babu usiku ndizo ambazo taratibu zilikuja kuchukuliwa na kutiwa katika maandishi na kufanya riwaya ya Kiswahili na pengine ya kiafrika.

Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba riwaya ya Kiswahili inatokana na Waswahili wenyewe kupitia nyanja zao za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni (Wamitila, 2008). Haya yanatokana na hali halisi ilivyo ambapo tunaona riwaya zikitungwa na kusawiri maisha halisi ya jamii katika mahusiano yao ya kila siku. Suala la kuja kwa wageni lilikuwa na mchango muhimu wa kusaidia katika kuifanya riwaya ya Kiswahili kuingizwa katika maandishi na hatimaye kuifikia jamii pana zaidi nje na ndani ya Tanzania.

## 2.2 Dhamira katika Riwaya ya Kiswahili

Utafiti kuhusu dhamira katika riwaya ya Kiswahili umefanywa na wataalamu mbalimbali ambao walikuwa na malengo tofautitofauti.

Mlacha (1989) aliandika makala juu ya matumizi ya sitiari katika riwaya ya Rosa Mistika na kutoa hitimisho kuwa sitairi zilizotumika katika riwaya husika zimesaidia sana katika kujenga dhamira hasa ile ya malezi. *Rosa Mistika* ni riwaya ambayo wazazi hasa baba anaonekana kuwa ni mtu mwenye msimamo mkali kuhusu maisha ya watoto wake na kamwe hakutaka kuona binti zake wakifuatana au kusimama na kuzungumza na mwanamme. Watoto wake waliishi katika maisha ya taabu wakiwa nyumbani na chini ya uangalizi wa wazazi lakini mara Rosa alipohitimu na kwenda kusoma mbali na nyumbani alikuwa huru kufanya mambo yake bila kukatazwa na wazazi. Alifanya mambo mengi kwa uhuru lakini baadae yalimletea shida kubwa na kuishia kujinyonga. Makala ya Mlacha (ameshatajwa) ilifungua uelewa wetu na kutufanya nasi kuwa makini tulipokuwa tunasoma riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* kumakinikia mbinu za kisanaa zikiwemo sitiari ili kuweza kupata dhamira vizuri. Ingawa sisi hatuchunguzi mbinu za kisanaa lakini ni wazi kuwa hatuwezi kuzipata dhamira bila kutafsiri matumizi ya mbinu za kisanaa.

Miongoni mwa wataalamu walioshughulikia dhamira karika riwaya ya Kiswahili ni Mbatiah (1998) ambaye alichunguza juu ya mienendo mipya katika utunzi wa Euphrase Kezilahabi kupitia riwaya zake za *Nagona* na *Mzingile*. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa *Nagona* na *Mzingile* ni riwaya ambazo zimekuja na dhamira mpya ambazo katika jhali ya kawaida zimekuwa hazisikiki au hazijadiliwi katika riwaya kongwe. Miongoni mwa dhamira hizo mpya ni ile ya kuhoji juu ya

maana ya maisha na kutoa hitimishi kuwa maisha hayana maana yoyote. Pia, riwaya hizi zimekuwa zikihoji juu ya uwepo wa Mungu na ukweli kuhusu dini kutaja kwa uchache. Mambo haya kwa pamoja yamezifanya riwaya hizi kuleta dhamira mpya ambazo awali hazikuwa zikipewa nafasi katika jamii. Maelezo haya ni mazuri na yana mchango katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa maana kwamba Shaaban Robert ni mtunzi ambaye yeye anaandika juu ya dhamira kinzani na zile za Euphrase Kezilahabi na hivyo tumeyachunguza kwa kina mawazo ya Shaaban Robert ili kuthibitisha ni kwa kiwango gani hayahusiani na yale dhahania ya Euphrase Kezilahabi.

Naye Shivji (2002) aliandika utangulizi wa riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* ya mwandishi Chachage Seith Chachage ambayo dhamira yake kuu ni masuala ya soko huria. Katika utangulizi huo amebainisha kwamba soko huria ni kitu ambacho hakiko sawa na kamwe hakiwezi kuwa huria kwa wananchi wote wa mataifa yote duniani. Mataifa yaliyoendelea huwa ni watu ambao ni wajanja sana na wameshapiga hatua kubwa za maendeleo katika nyanja za teknolojia, elimu na mitaji ikilinganishwa na nchi zinazoendelea ambapo nchi ya Tanzania ni mojawapo ya nchi hizo. Kutokana na hali hii ni dhahiri kuwa mataifa yaliyoendelea ndiyo ambayo yataendelea kufaidi soko huria kuliko nchi ambazo ni za ulimwengi wa tatu. Mataifa ya Ulaya na Marekani ambayo ndiyo yaliyoleta sera ya soko huria, yalifanya hivyo kwa makusudi yakitambua kwamba yatanufaika zaidi na soko huria kuliko mtu mwingine yoyote kutoka nchi masikini ambazo hapo awali zilikuwa ni makoloni ya Wazungu. Katika hali ya kawaida haiwezekani nchi zilizotoka katika hali ya kutawaliwa na rasilimali zake kuchukuliwa kwa maslahi ya wageni na kisha kuelezwa kuwa sasa

zinatakiwa kushindana katika soko huria. Jambo hili haliwezekani hata kidogo bali ni janja ya Wazungu kutaka kuendeleza unyonyaji waliokuwa wakiufanya katika kipindi cha ukoloni.

Maelezo haya yametusaidia katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa sababu riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* imeandikwa katika miaka ya hivi karibuni wakati ambapo ukoloni mkongwe umekwisha na ile ya *Siku ya Watenzi wote* iliandikwa katika kipindi cha utawala wa kikoni. Hii itatusaidia, pamoja na mambo mengine, kubaini kama yaliyosemwa au kusawiriwa katika riwaya ya *Siku ya Watenzi wote* bado yana nafasi katika ulimwengu wa leo wa utandawazi.

Pia, Mwaifuge (2006) alifanya uhakiki wa dhamira ya rushwa katika riwaya ya *Kitu Kidogo Tu*. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kuwa jamii ya Watanzania katika kipindi hicho waliifanya rushwa kama sehemu ya utamaduni wa maisha yao ya kila siku na hivyo kutokuwa tayari kupambana nayo. Ilifikia mahali watu wakawa hawafanyi jambo lolote mpaka wametoa au wamepokea rushwa ambayo ilifahamika kama kitu kidogo tu. Sambamba na hilo, pia mtaalmu huyu ameleza kwa kirefu juu ya athari ya rushwa katika jamii kuwa inachangia katika kudumaza maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla. Ni kutokana na vitendo vya rushwa ndipo barabara ambazo zipo chini ya kiwango hujengwa na kuipa serikali hasara kubwa ya kupoteza fedha za walipa kodi.

Kimsingi, maelezo ya mtaalamu huyo yametoa mchango muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwani suala la rushwa linajitokeza pia katika riwaya teule ambapo ni ukweli kwamba rushwa imekuwapo katika jamii kwa kipindi kirefu sana. Hata

hivyo, rushwa za sasa ni kubwa sana ikilinganishwa na zile ambazo zimekuwa zikifanyika katika miaka ya akina Shaaban Robert na muktadha mzima wa riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*. Mawazo haya tumeyachukua na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu.

Naye Khamis (2007) aliandika makala juu ya utandawazi au utandawizi, jinsi lugha ya riwaya mpya ya Kiswahili inavyodai na kufanikiwa kubainisha mambo mbalimbali. Anaeleza kuwa riwaya mpya ya Kiswahili ikiongozwa na zile za Kezilahabi za *Nagona* na *Mzingile*, *Ziraili na Zirani* ya Mkufya, *Babu Alipofufuka* na *Dunia Yao* za Saidi Ahmed Mohamed na *Binadamu* ya Wamitila zinaeleza bayana kuwa utandawazi ni kitu hatari kwa maendeleo ya nchi zinazoendelea. Wawekezaji huja na lugha laini ya kwamba wanawekeza mitaji yao na hivyo wapewe kipindi cha kutolipa kodi na mpaka pale biashara inatakopoanza kufanya vizuri ndipo waanze kulipa kodi. Wengine wameonekana kuwa sio waaminifu kwani baada ya kipindi cha kusamehewa kulipa kodi kwisha hufunga au huuza biashara zao kwa watu wengine kisha nao kuomba msamaha wa kodi kwa kipindi kingine cha miaka kadhaa. Huu ndio mchezo wa wawekezaji ambao kazi yao ni kuchuma na kujaza matumbo yao na kuziacha nchi za Afrika katika lindi la umasikini. Maelezo haya tumeyachukua na tumeyatumia katika kukuza na kusukuma mbele maarifa juu ya utafiti wetu.

Adam (2014) alifanya utafiti juu ya dhamira za kijamii na kiutamaduni katika riwaya za *Kuli* na *Vuta N'kuvute* za Shafi Adam Shafi. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kuwa riwaya teule zimetoa mchango muhimu katika kufunza na kuhifadhi masuala ya kijamii na kiutamaduni katika jamii. Miongoni mwa dhamira za kijamii alizozibainisha ni pamoja na uongozi, mapenzi, nafasi ya mwanamke,

umoja na mshikamano, kuheshimiana, kuthamini utu wa binadamu na wivu. Matokeo ya utafiti wake huu ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu ambao nao unachunguza dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* ambapo ilitusaidia katika kuona kama dhamira kama hizo zinapatikana katika riwaya teule. Tofauti na utafiti wetu, utafiti wa Adam (ameshatajwa) ulikwenda mbali zaidi na kuonyesha pia vipengele vya mbinu za kisanaa vinavyojiytokeza katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi.

## 2.3 Kazi Tangulizi juu ya Riwaya za Shaaban Robert

Riwaya za Shaaban Robert zimetafitiwa na wataalamu mbalimbali akiwemo Sengo (1973) amabaye alihakiki riwaya ya *Utu Bora Mkulima* na kueleza kuwa riwaya hii inahusu utu wa binadamu. Dhamira ambazo aliziona kuwa zinajitokeza katika riwaya hiyo ni haki na usawa, kuepuka dhuluma, kuwapenda na kuwasaidia watu wenye uhitaji na kuthaminiana miongoni mwa wanajamii. Maelezo haya tunakubaliana nayo bila tatizo lolote kwani hata jina lenyewe linaonyesha kuwa ni riwaya inayozunguma juu ya utu wema na upole. Ingawa utafiti huu ni tofauti na wetu kwa maana ya uchambuzi wa vitabu kuwa ni tofauti lakini mambo mengine ya msingi yanafanana sana na utafiti wetu. Kazi ya Sengo (ameshatajwa) imetusaidia sana katika kufungua uelewa wetu na kuweza kutimiza malengo mahususi ya utafiti wetu.

Kezilahabi (1976) alifanya utafiti na kuandika tasinifu ya Shahada ya Uzamili ikiwa na anuani, “Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya.” Pamoja na mambo mengine, amebainisha kuwa, riwaya nyingi kama sio zote ni riwaya ambazo zinaweza kusomwa na watu wa jamii mbalimbali nab ado zikayasiwiri maisha yao hata kama ni sehemu zenye utamaduni tofauti. Katika moja ya maelezo yake alimwita Shaaban

Robert kuwa ni “mlimwengu,” yaani mtunzi mwenye ujuzi wa kiwango cha juu ambaye kazi zake za riwaya, mashairi, insha na maghani zinaakisi jamii pana duniani kote na si jamii ya Waswahili wa Tanga peke yake bali na nchi nzima ya Tanzania. Ingawa utafiti huu ni tofauti na wa kwetu lakini tumeondoka na maarifa kwamba wakati mwingine ili kumuelewa au kuelewa kazi za Shaaban Robert vizuri ikiwa ni pamoja na *Siku ya Watenzi Wote* ambayo sisi tumeitafiti.

Mohamed (2006) aliandika makala juu ya mtindo katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* na kuvutiwa sana na mtindo wa uwili ambapo kila kitu kinapotajwa basi hutajwa na cha upande wa pili wa kitu hicho. Matumizi haya yanabainika pale ambapo kikitajwa kitu kama msikiti basi na kanisa pia litatajwa, shehe na pardi, mwanamke na mwanaume, mwema na muovu na mjanja na mjinga. Mtindo wa aina hii hutoa hamasa kwa wasomaji kuendelea kuisoma riwaya husika ili wafike mwisho na hatimaye wabaini dhamira zinazoakisiwa ndani ya riwaya husika. Mawazo haya tumeyachukua na kuyafanyia kazi katika tasinifu yetu ambayo haikuwa inatazama mtindo lakini tumeweza kupata data ya kutosha na pia kuchambua dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*.

Chuachua (2011) alifanya utafiti na kuandika tasinifu iliyokuwa na mada juu ya Itikadi katika riwaya za Shaaban Robert. Utafiti huu ulihusisha itikadi katika riwaya husika na kufanikiwa kubainisha aina kadhaa za itikadi ikiwa ni pamoja na kuheshimiana na kuheshimu imani na dini ya mtu mwingine. Shaaban Robert anaziona dini zote kuwa ni kitu kimoja na hivyo anasisitiza juu ya watu kuungana na kushirikiana katika shida na raha badala ya kutumia muda mwingi kutupiana kejeli na kudhalilisha dini na imani ya mtu mwingine. Kimsingi, Shaaban Robert ni mtu

ambaye anapenda kuona jamii inakuwa kitu kimoja ili kuweza kupata nguvu ya kujiletea maendeleo. Tumeyachukua mawazo haya na kuyafanyia katika tasifu yetu iliyolenga kuchunguza dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi wote*.

## 2.4 Mkabala wa Kinadharia

Katika sehemu hii tumeiwasilisha na kuitolea maelezo nadharia ya Saikolojia Changanuzi ambayo ndiyo tuliyoitumia katika uchambuzi wa data za utafiti huu.

### 2.4.1 Nadharia ya Saikolojia Changanuzi

Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ni moja kati ya nadharia mama katika ulimwengu wa fasihi na masuala mbalimbali ya kijamii hasa yanayohusiana na akili ya binadamu. Tunasema ni nadharia mama kwa sababu ni wazi kuwa hakuna jambo ambalo linafanywa bila ya kutumia akili. Hii ni sawa na kusema kuwa, mwandishi anapoandika kazi ya fasihi lazima atumie akili ili kuifanya kazi yake iwe na mantiki. Pia, msomaji wa kazi ya fasihi naye pia anatumia akili pale anaposoma kazi fulani ili aweze kuelewa ni dhamira au jambo gani linaloelezwa kupitia kazi husika ya fasihi (Wamitila, 2002). Kimsingi, nadharia ya Saikolojia Changanuzi iliasisiwa na Sigmund Freud mnamo mwaka 1896 ikichambua mambo makubwa matatu ambayo ndiyo yanatawala maisha ya binadamu (Sherwood, 2006). Mtaalamu Freud anaeleza kuwa binadamu ni kiumbe ambaye maisha yake yanatawaliwa na wasiwasi, raha na mahitaji. Katika mahitaji haya matatu, hitaji la raha au starehe linatajwa kuwa ndio kubwa kuliko mahitaji mengine.

Kimsingi, raha inayorejelewa katika nadharia hii ni ngono ambapo inaeloezwa kuwa, binadamu wote huanza kuipata starehe hii pale tu wanaponyonya matiti ya mama

zao. Matiti ya mama hutazamwa kama uume na mdomo wa mtoto huchukuliwa kama uke. Hivyo, kadri mtoto anavyonyonya kutoka kwa mama yake ndivyo anavyoipata starehe hiyo na huingia katika saikolojia au akili yake na pale anapofikisha umri wa kuoa basi huoa mwanamke ambaye atamtimizia raha hiyo. Vile vile kwa mtoto wa kike naye anapofikisha umri wa kuolewa naye huolewa ili kuweza kukidhi haja hiyo. Kwa wale ambao hawajaoa au kuolewa lakini tayari wameshafikisha umri huo basi nao hutafuta njia za kutekeleza haja hiyo. Hii inaonyesha kuwa upo ukweli kuwa hitajio hili ni la msingi sana katika maisha ya binadamu (Bowman, 2003).

Inaendelea kuelezwa kwamba suala la raha ya ngono katika maisha ya binadamu hujitokeza tangu utotoni kwa kutumia matendo mbalimbali yanayofanywa na mtoto akiwa mdogo. Mtoto mdogo ambaye anatoa haja ndogo au kubwa kila mara anatajwa kuwa atakuwa ni mtu ambaye anapenda sana ngono katika maisha yake ya ukubwani na yule ambaye anaona vigumu kutoa haja hizo, yaani yule ambaye anajizuia kutoa haja hizo basi hutajwa kuwa atakuwa ni mtu ambaye ni mnyimi katika tendo la ngono (Chapman, 2011). Kwa hakika, yapo maelezo mengi ambayo yanaelezea kuhusu hitajio hili la binadamu lakini itoshe kusema kuwa hili ni hitajio muhimu katika maisha ya binadamu.

Suala jingine ambalo linatajwa kuwa linamsumbua sana binadamu ni wasiwasi katika maisha ambapo hii inatokana na binadamu kutokuwa na uhakika wa maisha yake ya kesho. Ni ukweli uliokuwa wazi kuwa kila binadamu atakufa na kufarikiana au kutengana na dunia. Hata hivyo, hakuna mtu ambaye ana uhakika na siku ya kufariki na hivyo kuishi katika maisha ya hofu. Jambo hili huwasukuma baadhi ya watu kutofanya mambo ya maendeleo lakini wapo ambao wanautumia vizuri

wasiwasi huo kufanya masuala ya maendeleo kwa lengo la kuwaachia urithi watoto wao kama ikitokea siku moja wao wazazi wamefariki na kuondoka duniani. Sambamba na wasiwasi kuhusu uhai pia binadamu ni mtu mwenye wasiwasi kuhusu kazi yake, usalama wake, mnahusiano yake, mali zake, hali yake kama ni masikini au tajiri na mambo mengine mengi yanayohusiana na hayo. Wataalamu wa Saikolojia wanasema kuwa, suala la kuwa na wasiwasi katika maisha ni jambo zuri kwani wasiwasi humpa mtu akili na maarifa katika maisha. Jambo ambalo halitakiwi ni kuwa na wasiwasi uliopitiliza ambao hugeuka na kuwa ugonjwa. Mtu mwenye wasiwasi uliopitiliza mara nyingi hushindwa kutimiza majukumu yake vizuri na kuwa katika hali mbaya kiuchumu na kiafya.

Jambo la mwisho ambalo linatajwa kuwa ni muhimu katika maisha ya binadamu ni mahitaji ya msingi kama chakula, malazi na mavazi. Kwa hakika haya ni mahitaji muhimu ambayo ndiyo yanamfanya binadamu aweze kuishi na kuonekana vile alivyo. Kimsingi, ili akili ya binadamu iweze kufanya kazi vizuri ni lazima binadamu huyo awe ameshiba kwa kula chakula cha kutosha chenye aina zote za vitamini zinazotakiwa katika mwili (Smart, 2007). Mtu ambaye ana njaa akili yake itakuwa haijatulia na hatakuwa na uwezo wa kufanya mambo yake vizuri kama inavyotakiwa. Vilevile, binadamu anapokaa katika makazi mazuri yenye kuvutia ni tofauti kabisa na yule ambaye anaishi katika maeneo ambayo ni mathalani katika mafuriko au eneo ambalo halina usalama. Mtu wa aina hii kila mara atakuwa anafikiria tu hali ya makazi yake na hasa kipindi cha mvua kama anapoishi ni sehemu ya bondeni. Hali hii hupunguza sana ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali katika jamii.

Kwa jumla, tunapoyatazama mambo haya matatu tunaona kuwa yanaingiliana na kukamilishana vizuri sana. Hakuna jambo ambalo linaweza kutajwa kuwa ni muhimu kuliko jingine (Duck, 2007). Yote yanategemeana na kukamilishana. Kwa mfano, ili mtu aweze kutimiza tendo la ngono vizuri ni lazima awe amekula na kushiba vizuri na ili aweze kupata chakula ni lazima wasiwasi juu ya kufa na njaa awe nao na ahakikishe analima au anatafuta chakula ili aweze kuendelea kuishi. Hivyo, matumizi ya nadharia hii katika utafiti wetu ni muhimu kutokana na ukweli kuwa riwaya ya Siku ya Watenzi Wote ina masuala mengi ya kisaikoljia. Kwa mfano, suala la ukoloni ambapo nchi zetu zilitawaliwa na Wazungu ni suala la kisaikolojia na hivyo kutumia nadharia hii kutawezesha kuchambua vema dhamira mbalimbali katika riwaya teule.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi na kubaini kuwa utafiti kuhusu dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi wote* bado haujafanywa. Hivyo, tukaona kuwa hili ni pengo la maarifa ambalo tukiliziba tutakuwa tumetoa mchango wetu katika taluma ya fasihi ya Kiswahili. Pia, katika sura hii tumewasilisha nadharia ya Saikolojia Changanuzi ambayo ndiyo iliyotumika katika kuchambua data za utafiti kutokana na hali halisi kuwa nadharia hii ni muafaka kwa kuchambua riwaya za Shaaban Robert ambazo zinaigusa zaidi saikolojia ya wasomaji.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya na kuchambua data. Mbinu hizo zimehusisha usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya data za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Pia, katika sura hii tumeeleza juu ya kuaminika na usahihi wa data pamoja na maadili ya utafiti.

## 3.1 Usanifu wa Utafiti

Kazi ya kitaaluma kama utafiti hufanywa kwa kuzingatia taratibu mbalimbali na moja kati ya taratibu hizo ni kueleza utaratibu mzima wa namna utafiti ulivyofanyika. Utafiti huu ni wa kimaelezo ambao umehusisha kukusanya data za msingi katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1968. Hii ni sawa na kusema kuwa usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani ambapo riwaya teule imechunguzwa katika kipengele cha dhamira na hatimaye kueleza uhalisia wa dhamira hizo katika jamii. Huu ni uchunguzi kifani ambapo kazi ya fasihi kama riwaya teule huteuliwa na kuchunguzwa kwa kina ili kupata data husika. Aina hii ya usanifu ni nzuri kwa sababu humpa mtafiti uhakika wa kupata data stahiki kwa muda mfupi na tena kwa gharama nafuu (Robson, 2007). Hii inatokana na ukweli kuwa mtafiti huwa na uhakika wa kupata data sahihi kwa sababu anazikusanya kutoka katika chanzo ambacho ameshaishakichunguza na kuona kuwa ni muafaka katika kumpatia data za utafiti wake. Hivyo, katika tasinifu hii tumetumia

usanifu wa utafiti wa uchunguzi kifani kwa kuwa ni muafaka katika kuwezesha kukamilika kwa utafiti huu.

## 3.2 Kundi Lengwa

Katika utafiti au jambo lolote lile ni lazima kuwa na walengwa wake mahususi na katika utafiti huu tunalo kundi lengwa ambalo si jingine bali ni riwaya teule kutoka kwa Shaaban Robert. Riwaya hiyo ni *Siku ya Watenzi Wote* ambayo imechunguzwa katika kipengele cha dhamira na kisha kuelezea uhalisia wa dhamira hizo kwa jamii ya leo. Licha ya kwamba riwaya hii imeandikwa zaidi ya miaka 50 iliyopita lakini tumeona kuwa ina dhamira ambazo zina uhalisia katika jamii ya leo na hivyo tukaona kuwa ipo haja ya kuitafiti.

## 3.3 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni sehemu ya watafitiwa ambayo huteuliwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kuwa ni kiwakilishi cha watafitiwa wote katika jamii au mahali au vitu husika (Kothari, 2008). Sampuli ya utafiti huteuliwa ili kufanya utafiti kuwa fanisi na wenye tija kwa sababu si rahisi kuweza kuwatafiti wanajamii au vitu vyote vilivyopo kwenye jamii na kukamilisha utafiti husika kwa muda uliopangwa. Hivyo, sampuli ya utafiti wetu ni riwaya moja inayoitwa *Siku ya Watenzi Wote* iliyoandikwa na Shaaban Robert na kuchapwa kwa mara ya kwanza mwaka 1968. Lengo la kuteua riwaya hii ni ili kuweza kupata data za utafiti na kufanikiwa kuziba pengo la maarifa lililobainishwa katika sura ya kwanza na ya pili.

Sampuli ya utafiti huteuliwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa sampuli hiyo ni sahihi kwa mujibu wa utafiti husika. Kitendo cha

kuteua sampuli hujulikana kama Usampulishaji na mbinu ya kuteua sampuli ya utafiti huu inajulikana kama usampulishaji lengwa. Hii ni mbinu ya kuteua sampuli kwa makusudi maalumu kwa imani kuwa kuwa hiyo ni sampuli muafaka kwa mujibu wa utafiti husika (Cohen na Wenzake, 2000). Kwa kupitia mbinu hii ya Usampulishaji tumeweza kuteua riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* na kufanikiwa kupata data zinazohusiana na dhamira kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu. Mbinu hii ni nzuri kwani imetuwezesha kupata data ambazo tulikuwa tunazihitaji kwa ajili ya kukidhi malengo ya utafiti huu.

## 3.4 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti huu umekusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi na upili na maelezo kamili yametolewa katika sehemu inayofuata.

### 3.4.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hazikuwahi kukusanywa na mtu mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu ambao sisi tumeufanya (Babbie, 1999). Data za msingi wakati mwingine hufahamika kama data ghafi yaani data ambazo bado hazijafanyiwa uchakataji wa aina yoyote ile. Hivyo, data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kutoka karika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* ya Shaaban Robert ambapo imetupatia data zinazohusiana na dhamira.

### 3.4.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti watangulizi na kuchapishwa katika vitabu, makala, tasinifu, majarida, magazeti, vipeperushi na katika wavuti na tovuti (Creswell, 2009). Data za upili hupatikana katika maktaba na

hivyo katika utafiti huu tulisoma machapisho katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kupata data ambazo zilitumika katika kushadadia hoja zilizoibuliwa na data za msingi.

### 3.5 Mbinu za Kukusanyia Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Maelezo kwa kila mbinu yametolewa katika sehemu inayofuata hapa chini:

#### 3.5.1 Usomaji Makini

Kusoma kwa makini ni mbinu ya kukusanya data kutoka katika matini ambayo ni ya kifasihi kama ilivyo katika utafiti huu au isiwe ya kifasihi (Young, 1984). Katika kukusanya data za utafiti huu tulizingatia hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuisoma riwaya teule zaidi ya mara tatu ili kuilewa inazungumzia dhamira gani. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kuainisha mada kuu na ndogondogo kuhusiana na dhamira za riwaya teule kwa mujibu wa tulivyosoma na kubaini. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kusoma tena na kuanza kudondoa sehemu ambazo tuliona kuwa zinaelezea dhamira fulani na kuandika katika sehemu ya mada husika. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kupanga data vizuri data zilizokusanywa kwa kuondoa zile ambazo zinajirudia na kuunganisha zile ambazo zilikuwa na ukaribu wa kimantiki. Baada ya kukamilika kwa hatua hizo ndipo sasa kazi ya uchambuzi wa data ikaanza.

#### 3.5.2 Upitiaji wa Nyaraka

Data fuatizi katika utafiti wowote ule ni muhimu sana kwa ajili ya kuwazipa nguvu data za misngi (Kothari, 2008). Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kwa

kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka ambapo tulisoma machapisho kuntu kuhusiana na mada ya utafiti wetu. Machapisho na maandiko tuliyoyapitia ni pamoja na tasinifu, vitabu, makala, magazeti na ripoti mbalimbali za ripoti ambazo zilipatakana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## 3.6 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kama ifuatavyo:

### 3.6.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data za utafiti ambazo zinahusiana na kazi za fasihi kama riwaya, tamthiliya, ushairi, semi na hadithi simulizi na hata andishi (Young, 1984). Baada ya zoezi la kukusanya data kukamilika tulianza kuchambua data kwa kuwasilisha madondoo yenye dhamira husika na kisha kuyachambua kwa namna ambayo inajibu maswali ya utafiti wetu (John, 2007). Mbinu hii ni muafaka kwa utafiti huu kwa sababu haukuwa unahusisha takwimu na hivyo kuwa rahisi kwa wasomaji kufuatilia mtiririko mzima wa matokeo ya utafiti.

## 3.7 Kuaminika na Usahihi wa Data

Data za utafiti huaminika kutokana na kukidhi taratibu maalumu za utafiti na katika utafiti huu tumejitahidi kuzingatia taratibu zote (Yin, 1994). Miongoni mwa taratibu zilizozingatiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia mbinu sahihi ambapo kwa mujibu wa utafiti huu tumetumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka ambazo ni muafaka kwa utafiti kama huu

wetu. Data hizo pia zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Saikolojia Changanuzi ambayo nayo ni muafaka katika utafiti huu.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia maadili yote ambapo tulianza kwa kuandaa pendekezo la utafiti na mara lilipo kamilika ndipo tulikukwenda kukusanya data na hatimaye kuanza kazi ya uchambuzi na uandishi wa tasinifu ikafuata. Utafiti huu ni wa maktaba na hivyo data zote za msingi na hata upili zilitoka katika machapisho na hivyo, tulijitahidi kuzingatia maadili ya kudondoa kile ambacho kipo katika andiko husika na si vinginevyo. Robson (2007) anaeleza kuwa, miongoni mwa mambo ambayo yanafanya utafiti kuwa sahihi na pia kuaminika ni kuzingatia maadili ya utafiti.

### 3.9 Hitimisho

Katika sura hii tumewasilisha mbinu za utafiti ambao kwa namna moja au nyingine ndizo zilizotusaidia katika kukusanya data za utafiti na pia kuzichambua. Mbinu zilizotumika katika kukusanya data ni usomaji makini na upitiaji wa nyaraka na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni riwaya moja tu ya Shaaban Robert inayoitwa *Siku ya Watenzi Wote*. Sura inafuata inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti ili kuweza kukamilisha malengo mahususi ya utafiti wetu. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo ni kuchambua dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi wote* na kuelezea uhalisia wa dhamira za *Siku ya Watenzi wote* kwa jamii ya leo. Uchambuzi wa data umefanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Kutokana na malengo mahususi kuwa na ukaribu wa kimantiki tumeona kuwa ni vizuri malengo mahususi yote mawili tuyaunganishe pamoja katika uchambuzi wa data na tumefanya hivyo katika sehemu inayofuata.

## 4.1 Historia ya Shaaban Robert na Muhtasari wa *Siku ya Watenzi Wote*

Shaaban Robert alizaliwa tarehe mosi mwezi Januari mwaka 1909 katika kijiji cha Vibamba mkoani Tanga na kufariki mwezi Juni mwaka 1962. Shaaban Robert ni mshairi, mwandishi wa riwaya na Insha kwa lugha adhimu ya Kiswahili. Shaaban Robert ni mwanataaluma na mwanafalsafa ambaye ambaye alikuja kujulikana kama baba wa Kiswahili na mshairi wa Taifa. Jina la “Robert,” lilikuwa ni jna la afisa mmoja wa Kiingereza katika serikali ya kikoloni ambaye alimuomba baba yake Shaaban Robert kumuita mwanae jina hilo. Mara baada ya mtoto huyo kuzaliwa ndipo akaitwa Shaaban Robert lakini majina ya baba yake Shaaban Robert ni Selemani Kifukwe.

Shaaban Robert alipata elimu yake ya msingi kuanzia mwaka 1922 mpaka 1926 na kufanikiwa kuwa mwanafunzi wa pili kwa ufaulu kati ya wanafunzi 11 waliohitimu

katika shule ya Kichwele ambayo kwa sasa inafahamika kwa jina la Uhuru Mchanganyio. Baada ya kuhitimu masomo, mwaka 1926 aliajiriwa kama afisa forodha katika sehemu mbalimbali za Koloni la Tanganyika mpaka mwaka 1946. Baadaye mwaka 1946 mpaka 1952 alihamishiwa katika ofisi ya wilaya ya Tanga na kufanya kazi kama afisa ardhi. Pia, Shaaban Robert alifanya kazi kwa karibu sana na Chama cha Tanganyika African National Union (TANU) na Baba wa Taifa mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kutokana na kipaji chake katika utunzi wa kazi za fasihi alipata tuzo kama vile Margaret Wrong Prize na Medal for African Literature.

Kwa hakika, Shaaban Robert alikuwa ni mtu mwenye mchango mkubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili na mpigania haki, usawa na utu wa binadamu ambaye anaheshimiwa sana na watu kutoka imani mbalimbali za Kiislamu na Kikiristo. Hii inatokana pia na jina lake kuwa ni la pande hizo mbili za dini ambapo Shaaban ni jina la Kiislamu na Robert ni jina la Kikiristo. Shaaban Robert alifanikiwa kuzaa watoto 10 na mke mmoja aliyefahamika kwa jina la Amina ambaye ametajwa katika kazi kadhaa za mashairi ya Shaaban Robert. Shaaban Robert ni mtu ambaye alipenda sana kujiendeleza kielimu na mwaka 1934 alitunukiwa Diploma ya fasihi na mwaka 1936-37 alitunukiwa cheti cha lugha ya Kiingereza. Hii inaonyesha kuwa Shaaban Robert alikuwa anafahamu lugha za Kiswahili na Kiingereza lakini kazi zake aliziandika kwa lugha adhimu ya Kiswahili (Historia hii imedondolewa kutoka kwa Ambrose, 2014).

Shaaban Robert aliandika kazi nyingi za fasihi na kwa kuwa hapa tunachunguza riwaya ni vizuri kutaja baadhi ya riwaya zake. Riwaya hizo ni pamoja na *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Adili na Nduguze*, *Utu*

*Bora Mkulima* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* na *Siku ya Watenzi Wote*. Katika utafiti wetu tumechunguza dhamira katika riwaya ya *Siku ya Waatenzi Wote* ambayo inazungumzia ujenzi wa jamii mpya mara baada ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika. Maisha katika kipindi cha utawala wa kikoloni yalikwa ni ya kinyonyaji ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na maadili na hivyo, mara baada ya uhuru kulipaswa kuanzishwa kwa taasisi ambazo zingesaidia sana katika kukuza utu wa binadamu ambao ulipokwa na serikali ya kikoloni. Riwaya hii ilichapwa kwa mara ya kwanza mwaka 1968 lakini maudhui yake yanaonyesha kuwa iliandikwa miaka michache kabla ya uhuru wa Tanganiyika.

## 4.2 Dhamira katika *Siku ya Watenzi Wote* na Uhalisia Wake

Kama ilivyokwishakuelezwa hapo awali kuwa dhamira ni mawazo au malengo ya mtunzi wa kazi ya fasihi ambayo anataka hadhira yake iyapate. Malengo hayo yanaweza kuwa ni makuu au madogomadogo na hapo ndipo tunapata dhamira kuu na dhamira ndogondogo (Njogu na Chimerah, 1999). *Siku ya Watenzi Wote* ni riwaya iliyoandikwa na Shaaban Robert na kupigwa chapa kwa mara ya kwanza mwaka 1968 ikiwa imejaa dhamira kuntu kwa mustakabali wa maendeleo ya jamii. Miongoni mwa dhamira hizo ni wasiwasi, ukoloni, malezi, umasikini, kodi kandamizi, kutimiz wajibu, usawa, utunzaji wa mazingira, elimu, nafasi ya mwanamke, uchumi, mafundisho ya dini na ukahaba na uvutaji wa bangi. Dhamira hizi zimechambuliwa moja baada ya nyingine kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Wasiwasi

Wasiwasi ni hali ya hofu anayokuwa nayo binadamu juu ya mustakabali wa maisha yake ambapo anakuwa hana uhakika na maisha yake. Suala la kuwa na wasiwasi ni

suala la kisaikolojia na linamkumba kila binadamu. Kila binadamu ambaye yupo hai basi kwa namna moja au nyingine ana wasiwasi juu ya mambo kadhaa kuhusu maisha yake ikiwa ni pamoja na afya yake, kukidhi mahitaji, usalama wake, uhai wake, kipato chake, watoto wake, mali zake na kazi au ajira yake kutaja kwa uchache. Mwandishi Shaaban Robert amesawiri dhamira hii katika riwaya ya *Siku ya Watenzi wote* na hapa tunadondoa kama ifuatavyo:

> Watu wawili walikuwa wanapita barabara ya Bagamoyo katika Dar es Salaam kwenda Forodhani. Walikwenda kama watu waliokuwa hawana uzito wa wasiwasi, ila walichukuliwa na uzuri wa mji uliojaa majengo mazuri na magari (uk.1).

Shaaban Robert ni msanii mashuhuri kutokana na uwezo wake mkubwa aliokuwa nao katika uteuzi wa maneno. Katika dondoo hapo juu anabainisha kwamba suala la kuwa na wasiwasi kama sifa ya binadamu ni jambo la kawaida lakini hakusema bayana kuwa wahusika katika dondoo walikuwa na wasiwasi au la. Matumizi ya maneno, "… waliokuwa hawana uzito wa wasiwasi," ni maneno yaliyoteuliwa kisanii kuonesha kuwa hakuna binadamu ambaye hana wasiwasi katika maisha yake. Vilevile, mwanzoni mwa dondoo ameanza na maneno "watu wawili walikuwa…" ikiwa ni maneno yaliyoteuliwa kwa kutumia ustadi wa hali ya juu sana. Hapa ina maana ileile kuwa binadamu wote wana wasiwasi katika maisha yao na kiwango cha wasiwasi ndicho ambacho kinatofautiana baina ya wanadamu.

Kwa kurejelea nadharia ya Saikolojia Changanuzi tunapata ufahamu kwamba wasiwasi ni miongoni mwa mambo ya msingi katika maisha ya binadamu kwani ni kutokana na wasiwasi alionao binadamu ndio humfanya kuweza kuchukua tahadhari muhimu katika maisha na kuyafanya maisha kuendelea mbele. Wasiwasi unapozidi

huwa ni ugonjwa lakini kuwa na kiwango cha katikati cha wasiwasi ni jambo ambalo linakubalika na ni muhimu katika ustawi wa maisha. Shaaban Robert kama tulikwishakusema kuwa ni mtaalamu ambaye ana uwezo mkubwa wa kuteua maneno, ameeleza vizuri katika dondoo la hapo juu, juu ya tiba ya wasiwasi nayo si nyingine bali ni kubadili mazingira. Haya tunayapata kupitia sentensi ya mwisho ya dondoo hili pale anaposema, "ila waliochukuliwa na uzuri wa mji uliojaa majengo mazuri na magari." Hii ina maana kuwa mtu ambaye anasumbuliwa sana na wasiwasi kiasi cha kuwa kama ni ugonjwa basi njia nzuri ya kuondoa wasiwasi ni kubadili mazingira na kwenda katika maeneo ambayo ni tofauti na yale aliyoyazoea. Kwa kufanya hivyo kutamfanya kupata fikra mpya juu ya mambo mbalimbali katika maisha ikiwa ni pamoja na lile lililokuwa likimpa hofu na mashaka na hatimaye kupunguza hali hiyo. Tunasema kuipunguza kwani si jambo linalowezekana kwa binadamu kuweza kumaliza hofu na wasiwasi katika maisha yake isipokuwa pale anapofariki dunia tu.

Dhamira ya wasiwasi kuwa ni sifa inayounda maisha ya binadamu ni suala ambalo lina uhalisia katika maisha ya binadamu kwani watu wote bila kujali hali zao za kipato au kiwango cha elimu, viongozi au hata wananchi wa kawaida. Kila mtu ana wasiwasi kulingana na eneo lake la uzoefu katika maisha. Ni kutokana na wasiwasi binadamu alionao ndio maana hii leo kuna maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia na lengo hasa likiwa ni kuhakikisha kuwa binadamu anakabiliana na wasiwasi alionao kuhusu maisha. Laiti kama katika maisha ya binadamu kusingalikuwa na hata chembe ya wasiwasi basi maendeleo yaliyopo leo yasingalifikiwa kwa kiwango tulichonacho. Dunia ya leo imepiga hatua kubwa

katika maendeleo ya vifaa tiba sababu hasa ni wasiwasi alionao binadamu kuhusiana na uhai wake. Kila kukicha anajitahidi kubuni na kugundua teknolojia ya hali ya juu ambayo itasaidia katika kuimarisha afya yake na aweze kuishi maisha marefu zaidi.

Sambamba na hilo, uhalisia wa dhamira ya wasiwasi katika jamii unaweza kutazamwa katika eneo la ulinzi na usalama ambapo tunaona serikali za mataifa mbalimbali duniani zikifanya uwekezaji mkubwa katika majeshi kwa lengo la kuyaimarisha ili kumtibiti adui mara atakapotaka kuleta madhara. Wakati mwingine tumeshuhudia baadhi ya mataifa yakipinga vikali nchi nyingine kuwa na silaha kali za nyuklia yote ikiwa ni hofu na wasiwasi kwamba ikiwa nchi nyingine zitamiliki silaha za nyuklia basi zinaweza kuhatarisha usalama wa mataifa makubwa duniani. Hivyo, hii ni mifano michache tu ambayo inaonyesha namna wasiwasi ni kitu ambacho kipo katika saikolojia ya binadamu na hata siku moja hakiwezi kukosekana katika maisha yake mpaka pale atakapoondoka duniani.

Shaaban Robert katika kuonyesha kuwa wasiwasi ni kitu ambacho kila binadamu anacho lakini kinatofautiana kiwango anasema:

> Wote wawili walikuwa watu wa umri wa kati wa maisha; wa kwanza alionyesha sura ya mtu aliyefanikiwa katika kadhia zake. Uso wake ulikuwa mkunjufu, macho yalikuwa makali na mepesi, taya zake zilikuwa imara… (uk.1).

Matumizi ya neno, “katika kadhia zake,” ni mfano mzuri wa kuonyesha kuwa kila binadamu ana wasiwasi katika maisha yake na yule ambaye atafanikiwa katika maisha ni yule ambaye kwa namna moja au nyingine anajitahidi kuushinda wasiwasi katika maisha. Kama tulivyosema, kuwa siyo jambo jepesi kuweza kuushinda

wasiwasi lakini kujitahidi kuupunguza ni hatua nzuri sana ya kufanikiwa katika maisha. Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba, wasiwasi ni dhamira hai katika maisha ya binadamu na ina faida nyingi na pia ina hasara zake. Faida hujitokeza pale binadamu anapojitahidi kutumia wasiwasi kama fursa ya kupiga hatua za juu zaidi za maendeleo na hasara hujitokeza pale ambapo binadamu anaacha wasiwasi umtawale na kuwa kama ni ugonjwa mkubwa mwilini mwake. Dhamira nyingine inayofuata ni ukoloni.

### 4.2.2 Ukoloni

Ukoloni ni hali ya nchi moja kuitawala nchi nyingine kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Ukoloni umetokea au umefanywa katika nchi mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na nchi za Afrika takribani zote zilitawaliwa katika karne ya 19 na 20. Ukoloni ulianza mara tu pale nchi za Ulaya zilipofanya kikao chao cha Berlin mwaka 1884/5 na kugawana ardhi ya nchi za Afrika na kuzifanya kuwa chini ya utawala wa kikoloni. Tanganyika ambayo ndiyo nchi ya Tanzania upande wa Bara ilitawaliwa na Mjerumani kuanzia miaka hiyo mpaka ilipofika mwaka 1919 ambapo Mjerumani alinyang’wanywa makoloni yake yote na kuwekwa chini ya uangalizi wa Umoja wa Mataifa na pale itakapoonekana koloni fulani sasa linaweza kujitawala lilipewa uhuru wake kamili. Tuone namna dhamira ya ukoloni inavyojitokeza katika riwaya ya Siku ya Watenzi Wote:

> “Miaka kumi kamili. Sina jamaa hapa! Baada ya mama yangu kufariki dunia na dada yangu alipoolewa akenda zake kuishi mashariki ya kazi, ilionekana hapana cha kunileta kwetu. Walakini nimekuja sasa nami nina hakika kuwa sitaondoka tena hapa kwa sababu yoyote katika dunia. Naanza kufahamu kweli ambayo habari zake nimezisikia miaka hii michache, lakini ambayo sikuamini hata kidogo zamani.”

> "Hm, Tanganyika sinvyo ilivyokuwa?"
>
> "Kama hivyo, ni pahali pa kutumia mtu miaka yake sasa. Ilikuwa si nchi ya uhuru, ufanifu, wala usawa katika miaka iliyopita" (uk. 1).

Dondoo hili linasawiri dhamira ya ukoloni ambapo inaonyesha kuwa wananchi hawakuweza kuishi kwa furaha katika nchi yao na baadhi yao waliamua kuondoka kwenda kuishi mahali pengine pale walipopata furasa ya kufanya hivyo. Kama tulivyosema, kuwa Shaaban Robert ni bingwa katika kuteua maneno ambayo ndani yake kunaelezwa mambo mengi, tunaona ikitokeza tena katika dondoo hili. Kitendo cha mhusika katika dondoo kuondoka na kwenda kuishi ughaibuni na kuiacha nchi yake kimebeba mambo mengi sana ya kuzingatia. Itakumbukwa kuwa ni katika kipindi cha ukoloni wananchi walinyang'anywa ardhi yao na kubaki wakiwa hawana ardhi ya kulima, walilazimishwa kufanya kazi katika mashamba ya wakoloni kwa ujira mgodo, walilipishwa kodi kubwa ambayo walikuwa hawawezi kuimudu, walikosa fursa za elimu, ajira, huduma nzuri za afya na makazi yaliyokuwa bora ikilinganishwa na wakoloni wenyewe na wasaidizi wao ambao walikuwa ni Wahindi na Waarabu. Haya ni mingoni mwa mambo machache ambayo wakoloni waliyafanya dhidi ya wananchi ambao hawakufaidi chochote kutokana na rasilimali za nchi zao.

Si hivyo tu, bali pia, dondoo linaonyesha kuwa wakoloni walichukua rasilimali za nchi ya Tanganyika na nyingine walizozitawala bila huruma na bila kizuizi chochote. Katika dondoo inaonekana kuwa mhusika aliondoka nchini na kukaa ughaibuni kwa zaidi ya mika 10 kama anavyosema mtunzi, "Miaka kumi kamili…" ikiwa na maana kuwa kama mwenye nyumba hayupo basi watu wengine tu ambao hawana uchungu

na nyumba husika watafanya watakavyo hata kama ni kuiharibu nyumba yote. Kutokana na ubabe walioutumia wakoloni katika kuhakikisha kuwa ukoloni wao unaimarika na wanaendelea kuchota rasilimali za nchi walizotawala haikiuwa jambo jepesi kwa wazawa kuweza kushinda na kuwafukuza wakoloni isipokuwa kwa maeneo machache tu kama Ethiopia ambapo Waitaliano walishindwa vita na hatimaye kuifanya Ethiopia kuwa miongoni mwa nchi chache ambazo hazikutawaliwa na wakoloni.

Katika kuendelea kuonyesha kuwa wakoloni hawakuwa watu wema bali wanyonyaji wa rasilimali za makoloni, katika dondoo mtunzi anasema, "Sina na jamaa! Baada ya mama yangu kufariki dunia na dada yangu kuolewa na kwenda kuishi Mashariki ya kati…" ni ushahidi tosha juu ya wakoloni kumaliza rasilimali za mataifa ya Afrika. Kinachosemwa hapa ni lugha ya falsafa ya hali ya juu ambayo inaonyesha kuwa kitendo cha "mama kufariki dunia na dada kuolewa nje ya nchi" ni ishara kuwa katika nchi hakuna tena rasilimali kwani zote zimechukuliwa na serikali ya kikoloni na kwenda kunufaisha nchi zao. Mataifa ya Ulaya leo hii ni tajiri na yanasifika kuwa yameendelea na yapo katika ulimwengu wa kwanza lakini ukweli kuwa ni utajiri walionao umetokana na nchi za Afrika. Tunapoitumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi tunabaini kuwa wanajamii walishaanza kukata tamaa kwa kuona kuwa rasilimali za nchi zao zinachukuliwa na wao hakuna chochote wanachokipata na ndio maana wengine wakaamua kwenda kuishi nje ya nchi pale walipopata fursa ya kufanya hivyo.

Kimsingi, suala la ukoloni katika jamii bado ni halisia kwani hata hivi sasa wakoloni wameendelea kuchukuwa rasilimali za mataifa ya Afrika kupitia ukoloni mamboleo.

Itakumbukwa kuwa imekuwa ni kawaida ya wakoloni kunyonya mali za mataifa ya Afrika na walianza tangu enzi za biashara ya utumwa na ilipoonekana kuwa imepitwa na wakati wakaanzisha ukoloni na baada ya ukoloni kwisha wakaanzisha ukoloni mamboleo. Kutokana na ukoloni mamboleo ndio haya tunayoyaona ya kulazimisha soko huria duniani ambapo mtu kutoka sehemu yoyote ile ya dunia anaweza kuwekeza mahali popote pale bila kubughudhiwa kama tu anao mtaji wa kufanya hivyo. Katika uhalisia ni vigumu sana kukutana na Watanzania ambao wanaweza kufanya uwekezaji mkubwa katika nchi za Ulaya na Marekani kwa sababu hawana mtaji na teknolojia ya kufanya hivyo. Hili linawezekana kwa wawekezaji kutoka nje ya nchi na hasa Ulaya na Marekani kwa sababu wao ndio wenye uwezo wa mtaji na teknolojia. Uwekezaji wanaoufanya ni wa kuwanufaisha wao wenyewe na mataifa yao na si nchi kama Tanzania. Hivi karibuni tumeona namna makampuni makubwa ya uwekezaji katika madini yanavyochukuwa rasilimali za nchi na kujinufaisha wao wenyewe na kuiacha nchi kama Tanzania ikiendelea kuwa masikini licha ya kuwa na utajiri mkubwa wa rasilimali nyingi kuliko hata nchi za Ulaya.

Tukiitazama nadharia ya Saikolojia Changanuzi tunapata uelewa kuwa jambo la msingi ambalo hivi sasa linatakiwa kufanywa ni pamoja Watanzania kujitambua kifkira na kuamini kuwa wao wanaweza kufanya mambo makubwa ya kuwaletea maendeleo bila kutegemea wahisani ambao hutoa masharti mazito yenye mrengo wa kuwanuifa wao na si nchi. Tumeona serikali ya awamu ya tano ikiwa inafanya mambo mbalimbali kwa kutumia mapato ya ndani lengi likiwa ni lilelile la kuhakikisha kuwa maendeleo ya kweli yanapatikana pale watu wanapojitambua na

kuamini kwamba wanaweza. Dhamira inayofuata ni malezi kama inavyowasilishwa hapa chini:

### 4.2.3 Malezi

Malezi ni dhamira inayojipambanua katika kazi mbalimbali za fasihi simulizi na andishi kutokana na nafasi yake katika jamii (Njogu na Chimerah, 1991). Ni ukweli ambao haupingiki kuwa, malezi ndiyo ambayo huifanya jamii kuendelea na kukuwa na pia kupata maendeleo ya kweli kwa watu wake. Taifa au jamii ambayo haina malezi mema kwa wanajamii wake ni rahisi sana kuyakosa maendeleo na kuwa ni taifa la watu waliokuwa hovyo. Nafasi ya malezi katika jamii imekuwa ni muhimu kiasi hata cha kila mtu katika jamii kuona kuwa ni wajibu wake kuwafunza watoto na vijana kuishi katika misingi inayokubalika katika jamii licha ya kuwa wapo baadhi ya wanajamii hivi sasa wanaliona suala la malezi ya watoto na vijana kuwa ni kazi ya wazazi na sio ya jamii nzima kama ilivyokuwa hapo zamani. Shaaban Robert anaisawiri dhamira ya malezi barabara kupitia dondoo lifuatalo:

> Aziz Aliuliza, "Madhulum mwenyewe ni nani?" Mwanamke mmoja aliyetorokwa na mume wake. Ana watoto watatu walio chini ya umri wa miaka minane kuwakimu. Amri imekwishakutolewa juu ya mume huyo ya kulipa shilingi thelathini kila mwezi. Mwanamke huyo hapati pesa moja na wala hataipata kamwe (uk. 3).

Dondoo hili linaonyesha kuwa mwanamke ndiye ambaye amepewa jukumu kubwa la kuhakisha kuwa watoto wanapata malezi mema ili baadae wawe raia wema katika nchi yao. Hili linabainika kupitia dondoo hapo juu ambapo inabainika kuwa baadhi ya wanamme huwakimbia wake zao au wale ambao wamezaa nao kutokana na sababu mbalimbali lakini kubwa ikiwa ni suala la wao kukosa mali au fedha za kulea

familia. Maneno kama, “mwanamke mmoja aliyetorokwa na mumewa,” yanaonyesha namna baadhi ya wanamme wanavyowatelekeza wazazi wenzao na kuwaachia mzingi mkubwa wa malezi kwa watoto. Mzingo mkubwa tunaousema hapa ni katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na kumudu gharama za maisha ambapo watoto wanahitaji kula, kulala, huduma za afya, mavazi na kupata elimu. Vitu vyote hivi vinahitaji kipato cha uhakika na kipato hicho hakiwezi kupatikana kutoka kwa mwanamke wa kawaida yeye peke yake bila kusaidiana na mumwe wake.

Dondoo linaendelea kuonyesha kuwa wanamme hata wanapoamriwa kisheria kulipia gharama za malezi ya watoto huwa hawatekelezi jambo ambalo linaashiria kuwa ni mwanamke pekee ndiye ambaye anastahili kubebeshwa mzigo wa malezi ya watoto. Inaonekana vyombo vyenye mamlaka ya kisheria vinakuwa vimetoa maelekezo juu ya baba kutoa fedha za kujikimu watoto wakiwa kwa mama yao baada ya wao kutengana au baba kukimbia lakini bado akina baba wanawaachia wanawake peke yao na hawatimizi wajibu wao. Kisaikolojia, jambo hili linashiria kutokujitambua kwa baadhi ya wanajamii katika jamii zetu ndio maana hawatimizi wajibu wao. Malezi ya watoto ni kitu ambacho licha tu ya kuhitaji kufanywa na wazazi wote wawili lakini pia suala la kijamii na si la mtu mmoja peke yake.

Suala la malezi katika uhalisia kwa kiasi kikubwa linafanyika vizuri kwa maana ya wazazi wote wawili kushirikiana katika kulea watoto wao kwa hali na mali. Familia za aina hii hupata watoto ambao huwa na fursa ya kupata elimu na malezi bora kutoka kwa wazazi wote wawili na kujifunza mambo mengi zaidi ikilinganishwa na mtoto ambaye amekosa malezi ya wazazi wake wote wawili. Katika maisha ya siku

hizi tumeona ongezeko kubwa la watoto wa mitaani kwa sababu hawapati malezi kutoka kwa wazazi wote wawili na pale mzazi mmoja anapokosa uwezo wa kuwapatia mahitaji muhimu, watoto huchukua uamuzi wa kwenda mtaani kutafuta maisha na hatimaye kuwa ombaomba. Katika maisha ya mtaani watoto hukumbana na changamoto nyingi na nyingine huwa ni za kikatili lakini kwa sababu wapo mtaani inakuwa ni vigumu kusaidiwa na wao wenyewe huzoea hali hiyo na kuona kuwa ni sehemu ya maisha yao.

Kiuhalisia suala hili linaweza kutatuliwa kwa wanajamii kuendelea kuelimishana juu ya umuhimu wa wazazi wote kushirikiana katika malezi ya mtoto au watoto na inapotokea wazazi wametengana lakini katika malezi ya watoto bado wanaweza kuendelea kushirikiana ili kuhakikisha mtoto au watoto wanakuwa katika misingi inayokubalika katika jamii. Malezi kwa watoto ni tukio la kisaikolojia na linafanikiwa tu pale ambapo mzazi mwnyewe anakubali wajibu huo na kuutekeleza kwa vitendo (Mlacha, 1987). Wakati mwingine, matumizi ya vyombo vya sheria yanaweza yasimuonyeshe mzazi umuhimu wa kumlea mwanae yeye mwenyewe lakini alikubali jukumu hilo kisaikolojia inakuwa ndio njia madhubuti kuliko njia nyingine zote. Dhamira inayofuata ni umasikini kama tunavyoiwasilisha hapa chini:

### 4.2.4 Umasikini

Umasikini ni hali ya kutokuwa na kipato cha kutosha kuweza kumudu mahitaji muhimu katika maisha ya kila siku ya binadamu. Mahitaji ya kila siku ya binadamu ni chakula, malazi, mavazi na huduma za afya. Pale inapotokea mtu ameshindwa kumudu gharama za kupata mahitaji haya kwa ukamilifu wake basi mtu huyo ataitwa kuwa ni masikini (Mlacha, 1991). Huu ni umasikini wa kipato, lakini kuna aina

nyingine nyingi za umasikini kulingana na lengo la mtu anayeeleza maana ya umasikini. Wapo watu wengine wanaitwa kuwa ni masikini wa elimu kwa sababu tu hakupata fura ya kujiendeleza kielimu. Shaaban Robert katika *Siku ya Watenzi Wote* ameisawiri dhamira ya umasikini kama inavyotokeza katika dondoo lifuatalo:

> Wanawake kadha wa kadha ambao machozi huosha nyuso zao wamenambia thamani ya kutisha iliyofikiwa na sabuni sasa. Baadhi yao hunena, 'afadhali ningekwenda na njaa kuliko kuwa mchafu, lakini na watoto wanaolilia chakula mtu huwezaje kununua sabuni?' Kadhalika bei ya vyakula hupanda pia (uk.5).

Dondoo hili limewiana moja kwa moja na maana ya umasikini tuliyoitoa ambayo inadai kuwa, umasikini ni hali ya mtu kukosa fedha za kutosha kuweza kumudu mahitaji yake yote ya msingi. Shaaban Robert kwa ubingwa wake uleule wa kuteua maneno na kuyapangilia kwa namna nzuri yenye kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa analinganisha, sabuni na chakula kwamba vyote ni muhimu lakini kipi ni muhimu zaidi kuliko kingine bila shaka ni chakula. Hata hivyo, chakula bila ya kuwa nadhifu si itakuwa rahisi kuambukizwa magonjwa na hatimaye hata hamu ya kula chakula haitakwepo tena. Kimsingi, vitu vyote viwili ni muhimu na kinapokosekana kimoja huifanya jamii kuwa katika hali ya uduni na kukosa furaha. Umasikini ndio unaoifanya jamii ishindwe kuhakikisha kuwa mambo yake yanakuwa sawa kama inavyotakiwa kuwa.

Shaaban Robert katika dondoo hapo juu anaibua kigagaziko cha kisaikolojia ambapo kutokana na umasikini mzazi hasa mama anashindwa kuelewa ni kitu gani afanye aidha kununua chakula kwa ajili ya watoto aukununua sabuni. Suala la usafi hasa kwa wanawake ni suala nyeti la kiutamaduni lakini hapa mwanamke anatakiwa

kuchagua kati ya usafi na chakula kwa watoto ni kipi kitangulie kulingana na fedha alizonazo. Hatimaye kutokana na huruma kubwa aliyonayo mama kwa mtoto, hununua chakula na kuahirisha kununua sabuni lakini bado moyoni huendelea kuwa na mgagaziko wa kisaikolojia na hatimaye kuishi bila furaha.

Dhamira ya umasikini pia inajitokeza katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* kupitia katika katika dondoo lifuatalo:

> … Mpaka juzijuzi hivi aliishi katika kibanda kimoja kilichovunjwa sasa bila ya fidia na watoto wake, kwa kulipa kodi ya shilingi kumi kila mwezi. Lakini watu wa serikali walimwendea ikaonekana kuwa ilidhuru siha kuishi na kulala wengi katika kibanda hicho.
>
> Lazima apange vyumba viwili katika majengo ya serikali kwa shilingi thelathini kila mwezi. Yaani abakiwe na shilingi ishirini kwa ajili ya chakula kwa mwezi. Hali palikuwa na kitanda kimoja tu cha kulalia… (uk.3).

Dondoo hili linaonyesha umasikini katika suala la malazi ambapo kupata nyumba nzuri ni lazima uwe na fedha ya kulipa kodi kubwa sana kwani hata vibanda ambavyo vinaonekana kuwa havistahili kuishi wanadamu navyo pia ni ghali kwa mtu wa kawaida. Katika aya inayofuata ya dondoo, linatolewa suluhisho kuwa ni vizuri mhusika akahamia katika nyumba za serikali na kuchukuwa vyumba viwili ambavyo navyo gharama yake ni kubwa sana kwa mwananchi wa kawaida. Kwa maneno mengine, ni sahihi kusema kuwa mwananchi masikini hawezi kumudu gharama za kupangisha nyumba za serikali sasa atawezaje kumudu kodi katika nyumba za watu binafsi? Bila shaka hii ilikuwa ni serikali ya kikoloni ambayo yenyewe kazi yake ilikuwa ni kuwanyonya wananchi kila walichokuwa nacho. Serikali ya kikoloni

ilimtumikisha sana mwananchi na kumlipa ujira kidogo na hatimaye ujira huohuo mkoloni aliuchukua kupitia kodi nyingi ambazo ni kandamizi. Dhana ya kuendeleza umasikini kwa jamii za Kiafrika inajitokeza bayana tangu enzi za ukoloni mpaka leo. Kitendo cha kulipa ujira mdogo kwa wafanyakazi na kisha kukichukua kile kidogo chote kwa njia nyingine ni kuhakikisha kuwa jamii ya Waafrika inaendele kuwa duni tena duni kabisa.

Kimsingi, katika maisha halisia ya jamii, tumeona mara baada ya nchi kama Tanganyika kupata uhuru wake, serikali ifanya jitihada kuhakikisha kuwa makazi yanakuwa ni bure kwa wananchi wote na ilitaifisha majengo yote ambayo yalikuwa yanamilikiwa na serikali ya kikoloni na washirika wake na kuyafanya kuwa ni ya serikali. Ni katika majengo haya ndipo walikaa baadhi ya wananchi mara tu baada ya uhuru kupatikana na mpaka leo baadhi ya majengo hayo yapo na yamewekwa chini ya Shirika la Nyumba la Taifa pamoja wakala wa ujenzi Tanzania.

Katika hali ya kawaida si jambo jepesi kuumaliza kabisa umasikini kwa sababu suala la mahitaji huwa halidumu katika hali moja. Serikali za awamu zote nchini Tanzania zimefanya jitihada za kutosha katika kuhakikisha kuwa suala la umasikini linaondoka kabisa au linapungua kwa kiasi kikubwa. Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa umasikini katika jamii unadhitiwa kupitia Mkakati wa Kupunguza Umasikini na Kukuza Uchumi Tanzania (MKUKUTA), Mpango wa Kurasimisha Biashara Tanzania (MKURABITA), Mkakati wa Kukuza Uchumi Zanzibar (MKUZA) na Elimu Bila Malipo kama mikakati maalumu ya kupambana na umasikini. Jitihada zinaendelea kufanywa kupitia pia njia nyingine kama utolewaji wa mikopo midogomidogo kwa wajasiriamali wadogowadogo inayotolewa

kupitia vyombo mbalimbali vya fedha nchini Tanzania. Hii ni sehemu ya kupambana na umasikini ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia sana katika kupunguza umasikini katika nchi ya Tanzania.

Kwa upande mwingine, katika uhalisia imebainika kwamba, taasisi nyingi ambazo zinatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo zimekuwa zikitoza riba kubwa kiasi cha kuwafanya wananchi kufanya kazi ya kuzalisha fedha kwa ajili ya kunufaisha benki na taasisi husika huku wao wakiendelea kuwa masikini. Jambo hili limethibitika kupitia tafiti kadhaa ambazo tayari zimeshafanyika na mapendekezo kutolewa juu ya kupunguza riba inayotozwa na taasisi za fedha ili kumfanya mwananchi anufaike na mkopo anaoupata. Pia, matokeo ya tafiti hizo yanaonyesha kuwa, wajasiriamali wadogowadogo wanapatiwa mikopo bila ya kuwa na ujuzi wa kutosha wa masuala ya fedha hasa fedha za mkopo. Mapendekezo ni kwamba, jamii ya wajasiriamali wanatakiwa kupatiwa elimu ya kutosha kabla hawajapatiwa mkopo ili waweze kuutumia mkopo vizuri kwa manufaa yao lakini pia manufaa ya aliyewakopesha ili naye aendelee kuwepo na kutoa mikopo kwa watu wengi zaidi. Jambo jingine ambalo limeonekana kuwa ni kikwazo kwa wajasiriamali ni mkopo kutolewa na kutakiwa kuanza kurejesha ndani ya muda mfupi sana. Hii inawafanya wajasiriamali kutumia fedha hizo hizo walizopewa kufanya marejesho na kwa sababu kuna riba hulazimika kuchukuwa fedha nyingine zao za akiba na kupeleka kwenye taasisi iliyowakopesha. Hapa ndipo umasikini unapokuwa zaidi badala ya kupunguzwa na ndipo pakatolewa mapendekezo ya kutazama namna bora ya kutoa muda wa kutosha kwa wajasiriamali kuweza kufanya kazi kwanza kwa kutumia

mkopo waliopewa na ndipo marejesho yaanze kufanyika. Dhamira inayofuata ni wajibu na imewasilishwa katika sehemu inayofuata:

### 4.2.5 Wajibu

Kutimiza wajibu katika jamii ni kitu ambacho kinakwenda moja kwa moja na haki. Pale mtu anapodai haki fulani pengine haikutimizwa kwake na vyombo husika ni lazima naye pia ahakikishe kuwa anatimiza wajibu wake kwa sababu hakuna wajibu bila haki na hakuna haki bila ya wajibu. Kutimiza wajibu ni msingi wa maendeleo katika taifa na jamii yoyote ile iwayo kwani bila kutimiza wajibu jamii itakuwa masikini (Mlacha, 1996). Kwa mfano, mara baada ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika serikali ya awamu ya kwanza ilihimiza wananchi katika kufanya kazi ili kujenga jamii mpya. Kipindi hicho kulikuwa na kauli mbiu mbalimbali kama vile, “siasa ni kilimo,” “kilimo cha kufa na kupona,” “Ujamaa na Kujitegemea,” na katika serikali ya awamu ya tano yenyewe ina kauli mbiu ya “Hapa kazi Tu.” Kauli mbinu zote hizi lengo lake ni moja tu, kuhakikisha kuwa kila mtu anatimiza wajibu wake kwa lengo la kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu ya Tanzania. Shaaban Robert katika riwaya ya Siku ya Watenzi Wote anasema kwamba:

> … Mwanamke huyu hathubutu kumwandama mumewe mtoro kwa madai ya fedha hata kama ana wakati wa kutumia kwa kazi hii. Aliniambia, ‘Nusura angeniua mimi, au watoto, kama nilishikilia kumsumbua.’ Hifadhi? Hm, naam, hupatikana katika mazungumzo! Lakini iwapi ya matumizi? Jana tu mtu mmoja aliyetoroka mkewe, alirudi kwa ghafula, kumwona mkewe na watoto pamoja, aliingia kumpura mwanamke kwa makonde hata akawa hajifahamu na taabani. Mayowe ya watoto waliotishika yalileta majirani, mtu huyu alikamatwa akapelekwa gerezani… (uk.4-5).

Dondoo hili linaonyesha kuwa baadhi ya watu katika jamii na hasa wanaume wanakimbia kutekeleza wajibu wao kama baba katika familia na badala yake wanawaachia wanawake peke yao. Shaaban Robert ambaye ni bingwa wa kuteua na kutumia misamiati, katika dondoo hapo juu ametumia msamiati "mume mtoro" akiwa na maana ya mtu ambaye anakwepa wajibu wake na kumwachia mtu mwingine. Katika utamaduni wa Mwafrika ni mwanaume ndiye ambaye amepewa jukumu la kuhakikisha kuwa familia yake inapata mahitaji yote muhimu na mama anabaki kuwa ni msaidizi wa baba hususani katika malezi ya watoto na familia kwa jumla. Wanamme wengi hujisifu kuwa wao ni wanamme kweli kwa sababu wanaweza kumudu kutimiza wajibu wao kama baba katika familia. Kwa mwanaume ni ufahari kutimiza wajibu wake. Inapotokea baba anakimbia majukumu basi ujue hapo kuna tatizo kubwa ambalo inabidi litazamwe vizuri ili lidhibitiwe lisiwe kubwa.

Katika maisha halisi kumeibuka kundi la vijana ambao kazi yao ni kuwazalisha wanawake na wakati mwingine wasichana wadogo na kisha kuwatelekeza. Wanapoulizwa sababu kubwa ya kufanya hivyo hudai kuwa ni kutokana na hali ngumu ya maisha. Kwa hakika hili ni suala la kisaikolojia ambalo halina uhusiano wowote na ugumu wa maisha. Ugumu wa maisha huja kulingana na mtu mwenyewe anavyotaka lakini kama ni mtu mwenye kujitambua hutumia fursa mbalimbali zilizopo katika jamii kwa lengo la kujipatia kipato halali cha kumuwezesha kuihudumia familia yake. Vijana walio wengi wamekuwa ni watu wa kubweteka wasiopenda kujituma katika kufanya kazi na hivyo kushindwa kugharamia maisha ya familia zao na hatimaye hutoroka na kuwaacha wakiteseka. Dhamira inayofuata ni umuhimu wa elimu kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata hapa chini:

### 4.2.6 Umuhimu wa Elimu

Elimu ni ufunguo wa maisha ni usemi ambao umechukuwa nafasi kubwa katika maisha ya Watanzania walio wengi kwani hata katika baadhi ya shule hutumia msemo huu kama kauli mbiu ya shule (Mlacha, 1991). Usemi huu una maana kubwa sana katika jamii kwani hakuna mafanikio yoyote yanayoweza kutokea katika jamii bila ya elimu. Ni kutokana na elimu ndipo watu hupata maarifa na ujuzi wa kufanya shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Wanajamii na serikali kwa jumla imeona na inafahamu umuhimu wa elimu katika jamii na ndio maana serikali kupitia sera zake inatoa elimu bila malipo kwa wanafunzi wote kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba kwa shule za msingi na kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne kwa shule za sekondari. Pamoja na jitihada kama hizi lakini bado changamoto bado zipo lakini sio nyingi kama ilivyokuwa katika maisha ya akina Shaaban Robert. Katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* mwandishi anasema:

> Mwangaza ndani ya jengo ulikuwa hafifu, kwa sababu hapa palikuwa pahali paliposongwa na majengo mengine, na ingawa madirisha yalikuwa makubwa, nuru ilikingwa siku zote. Yusuff alipotazama upande ambao sauti ilisikiwa aliona watu kadha wa kadha. Katika watu hawa, palikuwa na masikini wanaume na wanawake waliokuja kutafuta msaada, watoto wao walikosa nafasi katika vyuo, wavulana na wasichana waliokuja kuadilishwa na kushauriwa juu ya mambo mbalimbali ya ulimwengu… (uk.10).

Katika dondoo hili tunamuona mtunzi akiisawiri barabara dhamira ya umuhimu wa elimu katika jamii. Katika dondoo hili anatujuza juu ya mambo mengi ikiwa ni pamoja na kwamba suala la wazazi kutaka watoto wao wapate elimu tena elimu ya Chuo Kikuu limeanza tangu enzi ya ukoloni. Kumbe jambo hili halikuanza leo bali ni la siku nyingi na hii ni kwa sababu wanajamii walitambua kuwa elimu ndio

ufunguo wa maisha kama tulivyotangulia kueleza hapo awali. Haya yanaelezwa na Shaaban Robert kupitia ujuzi na ustadi wake wa kutumia lugha ambapo anaifananisha elimu kuwa ni sawasawa na mwangaza na nuru ambayo kila mtu anatakiwa kuipata ili kuwa na mwelekeo mzuri katika maisha yake. Hata hivyo, anaeleza kuwa "licha ya madirisha kuwa makubwa bado nuru ilizuiwa ikashindwa kuingia ndani," kauli ambayo kwa hakika imejaa tafakuri kubwa kwa wasomaji wake. Serikali ya kikoloni haikutoa nafasi za elimu kwa Waafrika na hivyo kuwakosesha nuru muhimu katika kumulikia maisha yao (Mlacha, 1996).

Jambo jingine ambalo tunalipata katika dondoo hili ni kwamba nafasi za masomo katika elimu ya juu zilikuwa chache ikilinganishwa na mahitaji yaliyokuwepo. Hii ni sawa kabisa kwani wakoloni hawakuwa radhi kuona watu weusi wanapata elimu katika ngazi za vyuo sambamba na elimu katika ngazi za elimu ya sekondari. Wachache waliobahatika walipata elimu katika ngazi ya elimu ya msingi hususani madarasa ya awali mpaka darasa la nne. Hii ilikuwa ni njia ya kuwadumaza Waafrika kisaikolojia ili wajione kuwa wao hawana uwezo na hawastahili kusoma chuo Kikuu. Wakoloni walifahamu bayana kuwa wakiwaruhusu watu weusi wasome na kupata elimu ya juu watajitambua na kuwaondoa wakoloni. Azma hii ilifanikiwa kwa kiwango fulani lakini wale wachache waliopata nafasi ya kusoma huko Ulaya katika ngazi ya elimu ya juu ndio waliokuja kuongoza shughuli na harakati za ukombozi barani Afrika. Mfano mzuri wa viongozi hao wapigania uhuru ni Julius Kambarage Nyerere wa Tanzania, Kamuzu Banda wa Malawi, Nkwame Nkuruma wa Ghana, Keneth Kaunda wa Zambia na Jomo Kenyetta wa Kenya kuwataja kwa uchache tu. Katika uhalisia hivi sasa serikali imefanya jitihada kubwa ya kuongeza

fursa za masomo na wanafunzi wengi sasa hivi wanaingia katika elimu ya juu ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika kipindi cha ukoloni.

Jambo jingine kuhusu elimu linaloelezwa katika dondoo hili ni kuwa elimu haitakiwi kutolewa kwa ubaguzi wa kijinsia. Katika dondoo imebainishwa wazi kuwa wanafunzi ambao walikuwa wamekosa nafasi ya kujiunga na vyuo walikuwapo wanaume na wanawake. Anasema, “wavulana na wasichana waliokuja…” ikiwa na maana kwamba si wanaume tu ambao wanastahili kupata elimu na hasa elimu ya juu. Hapa mtunzi ametumia ule mtindo wake wa kipekee wa uwili kutujuza kuwa suala la elimu ya juu si la mwanaume pekee na kwamba mwanamke ni mtu wa kuolewa tu. Katika uhalisia tumona namna serikali imekuwa ikiongeza bajeti kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Jitihada hizi muhimu na inafaa zikaongezeka mara dufu ili kila mtu mwenye aweze kupata mkopo huo na kujiendeleza katika elimu ya juu.

Jambo jingine ambalo tunalipata katika dondoo hili ni kuwa ni watoto wa masikini ndio ambao hukosa fursa ikilinganishwa na watoto wa matajiri. Katika dondoo kuna kauli kwamba, “katika watu hawa, palikuwa na masikini wanaume na wanawake waliokuja kutafuta msaada…” Wakati watoto wa masikini wakikosa nafasi za masomo ndani ya nchi yao watoto wa matajiri wapo nje ya nchi wanasoma kwa gharama kubwa ambazo zingeweza kutumika hapa nchini katika kuimarisha miundombinu ya elimu ikiwa ni pamoja na madawati, vitabu na vitendea kazi vingine vingi.

Kimsingi, mambo ambayo yameelezwa katika dondoo hapo juu ni mambo sahihi kusuhu elimu kuwa ni ufunguo wa maisha. Kupitia nadharia ya Saikolojia changanuzi tunaweza kuona kuwa mwamko kuhusu elimu upo zaidi kwa upande wa wazazi badala ya wanafunzi wenyewe (Hassan, 2016). Suala la kutafuta elimu ni kitu cha lazima kama mtu huyo anataka kufanikiwa kimaisha na pia kufanikiwa katika kufahamu mambo mengi na kutumia ujuzi na maarifa husika katika kujikwamua kiuchumi. Ingawa wapo baadhi ya watu ambao hawajapata elimu katika mfumo rasmi lakini wamefanikiwa katika maisha. Wakati mwingine kitu kinachotakiwa ni kujituma na kufanya kazi kwa bidii kwani wapo waliopata elimu nzuri lakini hawajitumi na hivyo hawana maendeleo yoyote ya maana.

#### 4.2.7 Uzalishaji Mali

Uzalishaji mali ni kipengele muhimu katika maisha ambapo ndicho huwezesha aidha kufanikiwa au kutokufanikiwa katika maisha. Uzalishaji mali ni hutokea pale mtu au jamii inapoanzisha mradi fulani na kuanza kuutekeleza ili kuweza kupata kipato halali cha kuendeshea maisha yao. Katika jamii wanawake na wanaume wote wanashiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Zipo kauli kuwa mwanamke amekuwa akikandamizwa na mwanaume kwa muda mrefu na hivyo, ushiriki wake katika shughuli za uzalishaji mali sio mzuri ikilinganishwa na mwanaume. Maelezo haya kwa mtazamo wangu ninaona kuwa hayana mashiko ya kutosha kwani tumewaona wanawake katika sehemu nyingi wakishiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali (Mlacha, 1989). Shaaban Robert aliliona suala hili tangu enzi za ukoloni na kupitia Siku ya Watenzi Wote anasema:

> Ewaa. Twaleta mavazi na zana za kazi, lakini mavazi yenyewe huhitaji kutazamwa na kutengenezwa kwa uangalifu; vitambaa hutengenezwa mavazi mazuri ya wanaume, wanawake na watoto. Hii ndiyo kazi ambayo wanawake hutenda, na ujira wa wakati wao ni senti ishirini na tano… (uk.14).

Dondoo hili linaonyesha kuwa mwanamke ni mjasiriamali mzuri ambaye anafanya kazi za kuzalisha mali na kukuza kipato cha familia yake na hatimaye kuleta maendeleo ka tika taifa. Mara nyingi wanawake hufanya kazi kwa malipo kidogo lakini wanaonyesha kuwa ni watu ambao wapo tayari katika kujitolea kufanya kazi za uzalishaji mali hata kama ni kwa faida za wengine na wao kubaki kuwa watazamaji tu. Tumekuwa tukishuhudia katika maisha halisi ya jamii baadhi ya wanaume wakijibweteka na kumuacha mke akishughulika na shughuli za shamba lakini mazo yanapovunwa ni mwanaume ndiye anayeamua kila kitu kuhusiana na mazao hayo ambayo wala hakushiriki katika kuyazalisha. Kisaikolojia ni kawaida ya wanawake kujiona kuwa wao ndio wenye jukumu la malezi ya familia na huwa wapo tayari kwa lolote hata kuona mazao yote yanauzwa na mume wake bila ya yeye kunufaika nayo hata kidogo.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti ambazo zililenga kutimiza malengo mahususi mawili ya utafiti huu. Dhamira zilizochambuliwa na kuelezewa uhalisia wake ni pamoja wasiwasi, ukoloni, malezi, umasikini, kutimiza wajibu, umuhimu wa elimu na uzalishaji mali. Kwa jumla, riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* ni riwaya iliandikwa kwa ustadi mkubwa sana kiasi kwamba kila neno limebeba dhamira fulani. Matumizi ya mtindo wa uwili ndiyo

ambayo yanaifanya riwaya hii kuwa na upekee wa hali ya juu. Riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* imeandikwa siku nyingi kabla hata ya kupata uhuru ingawa ilikuja kupigwa chapa kwa mara ya kwanza baada ya uhuru na baada ya kifo cha Shaaban Robert lakini masuala karibu yote yanayoelezwa katika riwaya hii yana uhalisia katika maisha ya leo. Riwaya hii imetungwa na kuchapwa zaidi ya miaka 50 iliyopita lakini dhamira zake zina akisi uhalisia katika maisha ya jamii. Sura inayofuata inahusu hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo ya utafiti mzima kama ifuatavyo:

## 5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo yamewasilishwa kwa kuunganishwa kutokana na kuwa na ufanano wa karibu kimantiki. Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu likuwa ni kuchambua dhamira katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* na lile la pili lilikuwa ni kuelezea uhalisia wa dhamira za *Siku ya Watenzi Wote* kwa jamii ya leo.

### 5.1.1 Dhamira katika Riwaya Teule na Uhalisia wake

Katika kutimiza malengo mahususi ya utafiti huu tumewasilisha, kuchambua na kujadili jumla ya dhamira 7 ambazo ni wasiwasi, ukoloni, malezi, umasikini, kutimiza wajibu, umuhimu wa elimu na uzalishaji mali. Licha ya kwamba riwaya teule iliandikwa katika miaka 50 iliyopita lakini inaeleza dhamira ambazo bado zina manufaa makubwa kwa kizazi cha leo na hata kijacho. Hii ndiyo sababu kubwa ya Kezilahabi (1976) kumwita Shaaban Robert kuwa ni “mlimwengu,” yaani mtunzi ambaye anatunga kazi za riwaya zenye kuisawiri jamii yake ya sasa na ijayo na pia kuvuka mipaka na hata kusawiri jamii nyingine za nje za mataifa mengine.

Miongoni mwa dhamira zinazowasilishwa katika *Siku ya Watenzi Wote* ni pamoja wasiwasi. Suala la binadamu kuwa na wasiwasi katika maisha yake linatajwa kuwa

ni jambo la kawaida na ndio msingi wa maendeleo ya binadamu popote pale alipo. Binadamu anapokuwa na wasiwasi kuhusu maisha yake ya kesho yatakuwaje, ndipo anapopata msukumo wa ndani wa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili aweze kuyamudu maisha yake. Binadamu ambaye hana wasiwasi na maisha ni mtu ambaye muda wake wote wote huutumia kwa kujibweteka na hatimaye kuwa masikini au ombaomba katika jamii yake. Wakati mwingine, wasiwasi hutazamwa kama sehemu muhimu ya kumfanya binadamu kuwa na afya njema. Mtu ambaye anaishi bila ya wasiwasi mara nyingi huwa na mwili mkubwa ambao ni hatari kwa afya yake. Hata hivyo, wasiwasi haupaswi kuwa mkubwa kiasi cha kumkosesha mwanadamu amani kwani inaweza kuwa ni hatari kwa afya yake na hata kupoteza maisha. Uhalisia katika maisha unaonyesha kuwa watu wenye msongo mkubwa wa mawazo unaosababishwa na wasiwasi hupata madhara ya kiafya.

Suala la ukoloni ambalo linatajwa katika riwaya teule kuwa wakoloni walikuwa ni watu ambao walikuwa wanachukua rasilimali za makoloni na kupeleka katika nchi zao kwa manufaa yao wenyewe na kuziacha nchi masikini zikiendelea kuwa duni na masikini. Mawazo haya bado tunayaona yakiendelea hata leo kupitia ukoloni mamboleo ulioletelewa na utandawazi. Tumeshuhudia nchi za Afrika zikiingia katika mikataba yauchimbaji wa madini isiyokuwa na tija kwa nchi bali kwa masilahi ya wawekezaji kutoka nchi zilizoendelea za Marekani, Ulaya na Asia. Baadhi ya nchi kama Tanzania tayari imelingua suala hilo la kuibwa kwa rasilimali madini na tayari hatua stahiki zimeanza kuchukuliwa.

Suala la malezi katika jamii linatajwa kuwa ni muhimu sana katika kujenga kizazi chenye maadili katika siku za usoni ili kuwa na jamii yenye maadili. Malezi

yanayopendekezwa katika riwaya teule ni yale ya wazazi wote wawili yaani baba na mama kulea watoto wao. Wapo baadhi ya wazazi hasa wanaume ambao hutoroka au kutelekeza familia zao na kumuacha mama na watoto yeye mwenyewe. Jambo hili ni baya kwani si tu kwamba linakuwa ni mzigo mkubwa kwa mama kuchukua majukumu ya baba pia lakini kubwa zaidi watoto husika hukosa mwelekeo mzuri wa kimaadili na wakati mwingine huishia kuwa watoto wa mtaani. Uhalisia unaonyesha kwamba, kundi kubwa la watoto wa mtaani wanatokana na kukosa malezi mazuri mara baada ya wazazi wao kufarakana na kutengana.

Dhamira ya umasikini ambao ulikuwepo katika kipindi cha uhai wa Shaaban Robert bado pia inaendelea kuisadifu jamii ya leo ingawa kuna mabadiliko makubwa ikilinganishwa na wakati huo. Katika riwaya teule kunaonyeshwa kuwa jamii gharama za maisha ni kubwa ikilinganishwa na kipato cha wananchi na hivyo wengi wao kushindwa kumudu mahitaji yao kama chakula, malazi na mavazi. Tumeshuhudia katika riwaya teule familia kubwa ikiishi katika chumba kimoja au viwili tu ambapo watoto huchanganyika na watu wazima. Jambo hili linasababishwa na umaskini uliopo katika jamii. Hata hivyo, katika kipindi hiki tangu tulipopata uhuru mpaka sasa serikali imekuwa ikitoa mitaji midogomidogo kwa wajasiriamali ambao wengi wao ni wanawake na vijana kitu ambacho kinawasaidia sana katika kuimarisha maisha yao na kupambana na umasikini. Fursa hii haikuwepo katika kipindi ambacho Shaaban Robert aliishi na kufanya kazi katika serikali ya kikoloni ambapo waliopatiwa fursa hiyo ya kuwezeshwa walikuwa ni wazungu, wahindi na waarabu tu.

Kimsingi, suala la kutimiza wajibu miongoni mwa wanadamu ni suala muhimu katika kujiletea maendeleo. Kupitia riwaya teule tumeona baadhi ya wahusika

wakikimbia majukumu yao na hatimaye kutotekeleza wajibu wao. Hapo kale wanaume wamekuwa ni watu ambao huona fahari kubwa kwa kuweza kuhudumia fammilia zao kwa kuwakidhia mahitaji yao yote. Lakini wapo baadhi ya wanaume siku hizi huona ufahari kwa kutelekeza familia zao na kumuacha mama akihaha yeye peke yake katika kuwahudumia watoto wake. Jambo hili ni baya na halikubaliki katika jamii hata kidogo. Taasisi husika zinawachukulia hatua wahusika lakini ukweli ni kuwa hili ni suala la kisaikolojia ambapo jamii inapaswa kuelimishwa na kulikubali. Kuwachukulia hatua tu wahusika bila kutoa elimu haitasaidia sana katika kuwafanya wanajamii wote kutumiza wajibu wao kwa ustadi na umakini unaotakiwa. Hili linakwenda sambamba na dhamira ya kutoa elimu kwa jumla katika jamii ili kuwa na wataalaumu mbalimbali ambao wanaweza kuajiriwa na pia kujiajiri wao binafsi ili kuweza kujiletea maendeleo.

## 5.2 Hitimisho

Kwa hakika, Shaaban Robert ni mtu ambaye alikuwa na maarifa na maono ya mbali sana kwani anathibitisha kuwa maendeleo ya kweli katika jamii yatatokana na kukamilika kwa mambo yote hayo tuliyoyawasilisha hapo juu na hatimaye kufanya uzalishaji mali wenye tija. Uzalishaji hauewezi kutokea katika jamii ambayo haina mipango madhubuti, bado ina mawazo ya kikoloni, malezi ya jamii yake ni duni, wananchi hawatimizi wajibu, jamii haina wasomi na mwisho uzalishaji mali itakuwa ni ndoto isiyoweza kutimia. Kiuhalisia mambo haya ni sahihi na tumeona kwa baadhi ya wanajamii ambao wameepukana na sifa hizo na kujipamba na sifa za kujituma wakiwa na maendeleo makubwa ya kuweza kuigwa.

## 5.3 Mapendekezo

Tunapendekeza utafiti wa kuchunuguza fani katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* ufanyike ili kuweza kuibua utajiri mkubwa wa fani ya riwaya hii ya nguli wa fasihi na lugha ya Kiswahili Shaaban Robert.

Pia, tunapendekeza utafiti kama huu ufanywe katika riwaya nyingine za watunzi wengine wa riwaya kwa lengo la kulinganisha na riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*.

**MAREJELEO**

Adam, O. A. (2014). “Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kitamaduni katika Riwaya ya Kiswahili; Mifano kutoka *Kuli* na *Vuta Nkuvute*.” Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Haijachapishwa.

Ambrose, B. M. (2014). Kuchunguza Masuala ya Kisiasa katika Riwaya za Shaaban Robert: Mfano wa Kusadikika na Kufikirika.” Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Kisahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Bouman, Z. (2003). *Liquid Love: On the Frailty of Human Bonds*. Cambridge: Polity Press.

Chapman, H. M. (2011). *Love: A Biological, Psychological and Phisiological Study*. Rode Island: University of Rode Island Press.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: TATAKI.

Cohen, L. *et. al*. (2000). *Research Methods in Education* ($5^{th}$ end) London: Routledge.

Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Duck, S. (2007). *Human Relationships*. London: Sage Publication.

Hassan, A. M. (2016). "Kuchunguza Falsafa ya Mapenzi katika *Diwani ya Mapenzi Bora*." Tasinifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

John, L. (2007). *Critical Reading: A Guide*. In http://www. Brocku. Ca/English/jlge/criticalreadig. Html. Accesssed, 30th, October 2007.

Kezilahabi, E. (1976). "Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya." Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar ear es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Khamis, S. A. M. (2007). "Utandawazi au Utandawizi?: Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai." katika *Kiswahili*, Juzuu namba 70, Dar es Salaam: TUKI, Kur.47-66.

Kothari, C. R. (2008). *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques*. New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Madumullah, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Mbatiah, M. (1998), "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*," Katika *Mulika* namba 24, TUKI, Kur. 1-11.

Mkangi, K. (1995). *Walenisi*. Dar es Salaam: EAEP.

Mkufya, W. E. (1999). *Ziraili na Zirani*. Dar es Salaam: Hekima Publishers.

Mlacha, S. A. K. (1987). "The Portrayal of Cultural Conflict in Kiswahili Prose Fiction; A Structual Study of the Novels of Euphrase Kezilahabi." Phd. Thesis, University of London.

Mlacha, S. A. K. (1989). "The Use of Methaphor in Kezilahabi's Novel: *Rosa Mistika*," katika *Kiswahili*, *Juzuu namba 56*, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 25-35.

Mlacha, S. A. K. (1991). "Point of View as Stylistic Device in Kiswahili Novels." in *Kiswahili Vol. 58*, Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S. A. K. (1996). "Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya *Bwana Myombekere* na *Bibi Bugonoka*." katika, *Mulika* namba 23, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 24-35.

Mlacha, S. A. K. & Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohamed, M. (2006). "Mtindo katika Riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*." katika *Kioo cha Lugha*, *Juzuu namba* 4, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 1-12.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

Muhando, P. & Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonesho,* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. (1990). “Utunzi wa Riwaya ya Historia.” katika *Mulika* namba 22, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 1-10.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mwaifuge, E. S. (2006). “Fasihi ya Kiswahili na Rushwa Tanzania: Thomas A. R. Kamugisha na *Kitu Kidogo Tu*.” Katika, *Kioo cha Lugha, Juzuu namba 4*, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 39-45.

Njogu, K. & Rocha, C. (1999). *Ufudishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: JKF.

Robert, S. (1951). *Kusadikika*. London: Nelson.

Robert, S. (1951). *Adili na Nduguze*. London: Macmillan.

Robert, S. (1958). *Wasifu wa Siti Binti Saad: Mwimbaji wa Unguja*. London: Thomas.

Robert, S. (1967). *Kufikirika*. Nairobi: OUP.

Robert, S. (1968). *Siku ya Watenzi Wote*. London: Nelson.

Robert, S. (1968). *Utubora Mkulima*, Nairobi: Nelson.

Robert, S. (2003). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Robson, C. (2007). *How to do a Reserch Project*: *A Guide for Undergraduate Students*. Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Shivji, I. (2002). “Makuadi wa Soko Huria (Chachage, S. Chachage): Hotuba ya Uzinduzi wa Kitabu,” katika *Mulika* namba 26,

Sengo, T. S. Y. M. (1973). “Mtu ni Utu (G. Mhina).” Katika *Hisi Zetu*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (1977). “Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Umma.” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Sherwood, L. (2006). *Fundamentals of Physiology: A Human Perspective*. Belmont: Thomson Books.

Taib, A. H. (2008). “Mkabala wa Kiislamu katika Uchanganuzi na uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili.” *CHAKAMA*, kur. 133-141.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, (2002). *Bina-Adamu*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2$^{nd}$ eds.) Thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Surves and Research*. Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.